

UKURASA WA 2

**Anayedaiwa kinara mtandao dawa za kulevya atiwa mbaroni**

UKURASA 3



UKURASA WA 2

**Miamala simu yaongezeka asilimia 30**

UKURASA 5



**Kivumbi 16 bora AFCON**

UKURASA 22


# Nipashe

IJumaa Januari 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581567

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## MATOKEO KIDATO IV

# Wavulana wapindua meza 2023

UKURASA 2

Asilimia 89.36 wafaulu

Hisabati bado kikwazo



102 wafutiwa matokeo

Tatizo la matusi laendelea

Masomo ya sayansi ufaulu juu

Mkuu wa shule abambwa akisaidia wanafunzi



UKURASA WA 21

**MO SALAH RASMI AREJEA LIVERPOOL**

MOHAMED Salah amerejea England salama kupata matibabu kutokana na jeraha lake la misuli ya paja...

## Samia ataja sababu tano za kuwaleta wawekezaji Tanzania

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akinawishwa mikono na Rais wa Jamhuri ya Indonesia, Joko Widodo baada ya kupanda mti wa kumbukumbu katika viwanja vya Makazi ya Rais huyo Bogor jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 14



Saudia yafungua duka la pombe mara ya kwanza

# Wamiminika kumwomba msaada Rais baada ya mmoja kufanikiwa

UKURASA 2

MICHEZO **STARS YAWEKA REKODI, YAPONGEZWA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Wavulana wapindua meza 2023

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) limetangaza matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne na Maarifa yakionyesha wavulana kufaulu zaidi kulinganisha na wasichana.

Aidha, NECTA imefuta matokeo ya watahiniwa 102, akiwamo mmoja wa Maarifa, baada ya kufanya udanganyifu kwa baadhi kuingia na simu, kukutwa na notisi 'vibomu' na wengine kutazamiana. Pia mkuu wa shule amekamatwa akiwasaidia wanafunzi na hatua dhidi yake zimechukuliwa.

Tatizo la watahiniwa kuandika matusi limeendelea kujitokeza baada ya wanafunzi watano kufanya hivyo hatimaye matokeo yao kufutwa. Baraza pia limezuia matokeo ya watahiniwa 376 waliopata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya masomo yote au idadi kubwa ya masomo.

Wakati hayo yakijitokeza, NECTA imebainisha kuwa ufaulu wa somo la Hisabati umeendelea kuwa chini ya wastani kama ilivyokuwa mwaka 2022 licha ya kufikia asilimia 25.42kulinganisha na asilimia 20.08 ya mwaka 2022.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, akitangaza matokeo hayo jana mkoani Dar es Salaam, alisema watahiniwa 484,823 sawa na asilimia 87.65 ya waliofanya mtihani huo, wamefaulu.

"Wasichana waliofaulu ni 257,892 sawa na asilimia 86.17 wakati wavulana waliofaulu ni 226,931 sawa na asilimia 89.40. Mwaka 2022 watahiniwa waliofaulu walikuwa 476,450 (asilimia 86.78), hivyo ufaulu wa watahiniwa umeongezeka kwa asilimia 0.87 kulinganisha na mwaka 2022," alisema.



Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

Dk. Mohamed alisema watahiniwa 471,427 wa shule kati ya 527,576 wamefaulu, sawa na asilimia 89.36.

"Watahiniwa hao wamepata madaraja I, II, III na IV. Mwaka 2022 watahiniwa waliofaulu walikuwa 456,975 sawa na asilimia 87.7, hivyo ufaulu umeongezeka kwa asilimia 1.57. Pia kuna ongezeko la watahiniwa 14,452 sawa na asilimia 3.16 ya waliofaulu kulinganisha na mwaka 2022," alisema.

Dk. Mohamed alisema kati ya watahiniwa 471,427 waliofaulu, wasichana ni 250,147 sawa na asilimia 88.11 na wavulana ni 221, 280 ambao ni asilimia 90.81, hali inayoonyesha kuwa wavulana wamefaulu vizuri zaidi kuliko wasichana.

Kuhusu watahiniwa wa kujitegemea, alisema waliofaulu mtihani ni 13,396 sawa na asilimia 52.44 wakati mwaka 2022 walikuwa 19,475 sawa na asilimia 68.34 ya walifaulu mtihani huo. Kwa hiyo, ufaulu wa watahiniwa wa kujitegemea umeshuka kwa asilimia 15.90 kulinganisha na mwaka 2022.

**UBORA UFAULU**

Dk. Mohamed alisema ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata watahiniwa wa Shule unaonyesha kuwa waliopata ufaulu mzuri wa madaraja ya I, II na III ni 197,426 sawa na asilimia 37.42.

Kwa mwaka mwaka 2022, alisema kwa waliofaulu katika madaraja hayo walikuwa 192,348 sawa na asilimia 36.95, hali inayoonyesha kuwa ubora umeongezeka kwa asilimia 0.47 ikilinganishwa na mwaka 2022.

"Ubora wa ufaulu wa madaraja I-III ni mzuri zaidi kwa wavulana ikilinganishwa na wasichana. Wavulana ni 108,368 sawa na asilimia 44.47 na wasichana ni 89,058 ambao ni asilimia 31.37," alisema.

**UFAULU WA SHULE**

Dk. Mohamed alisema ufaulu wa shule katika makundi ya umahiri unaonyesha kuwa kati ya shule 5,343, shule 5,334 sawa na asilimia 99.83 zimepata wastani wa Daraja A-D ikilinganishwa na shule 5,169 sawa na asilimia 99.58 zilizopata wastani huo kwa mwaka 2022. Ongezeko hilo ni asilimia 0.25.

"Shule zilizopata wastani wa Daraja A-C zimeongezeka kwa asilimia 1.36 kutoka shule 1,870 sawa na asilimia 36.02 mwaka 2022 hadi shule 1,997 sawa na asilimia 37.38 mwaka 2023," alisema.

**UFAULU KIMASOMO**

Dk. Mohamed alisema katika masomo ya Sayansi ya Jamii watahiniwa waliofaulu masomo ya Civics, History na Geography ni kati ya asilimia 63.20 hadi 67.83.

"Katika somo la History ufaulu umeongeza kwa asilimia 1.19 na umeshuka kwa asilimia 2.21 kwenye somo la Civics na asilimia 1.78 kwenye somo Geography ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022.

"Masomo ya Sayansi ya Jamii yana bora wa ufaulu wa kati ya asilimia 30. 33 hadi asilimia 30.91 kwa watahiniwa waliopata ufaulu kati ya gredi A hadi C sawa na asilimia 45 hadi 100.

"Ufaulu waliopata Daraja A na B umeongezeka kwa asilimia 1.94 kwenye somo la Uraia, asilimia 1.07 somo la Historia na asilimia 1.51 Jiografia ikilinganishwa na mwaka 2022," alisema.

**MASOMO YA LUGHA**

Dk. Mohamed alisema katika masomo ya Kiswahili na Lugha ya Kichina yana ufaulu mzuri sana kwa Kiswahili ikiwa asilimia 96.80 na Kichina asilimia 91.36.

Alisema ufaulu watahiniwa waliopata Daraja A na B umeongezeka kwa asilimia 1.54 somo la Kiswahili na umeshuka kati ya asilimia 0.02 hadi asilimia 1.26 kwenye masomo ya Kiingezera, Kiingereza Fasihi na Lugha ya Kiarabu.

"Katika somo la Kifaransa asilimia ya waliopata Daraja A na B imeshuka kati ya asilimia 4.68 na 18.13 ikilinganishwa na mwaka 2022.

**MASOMO YA SAYANSI**

Dk. Mohamed alisema ufaulu wa watahiniwa waliopata Daraja A na B umeongezeka kwa kati ya asilimia 0.03 hadi asilimia 26.34 katika masomo ya Fizikia, Kemia, Uhandisi.

"Hisababti ni somo lenye ufaulu wa chini kwa watahiniwa waliopata Daraja A na B kwenye masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia japokuwa ni somo lenye asilimia kubwa ya watahiniwa waliopata gredi A ikilinganishwa na Fizikia, Kilimo, Uraia, Jiografia na Kiingereza," alisema.

**MASOMO BIASHARA**

Dk. Mohamed alisema watahiniwa waliofaulu somo la Commerce ni asilimia 81.02 na waliofaulu somo la Book-Keeping ni asilimia 78.62. Ufaulu wa somo la Commerce umeshuka kwa asilimia 2.90 na ufaulu wa somo la Book-Keeping umeshuka kwa asilimia 8.31.

VISIT
FREE ENTRY
INTL TRADE EXHIBITION ON FOOD & PROCESSING PLASTICS & PACKAGING

EXHIBITORS FROM AROUND 13 COUNTRIES

FOODPACK 2024
INTL FOOD & PROCESSING TRADE SHOW - EAST AFRICA

Products on Display:
Juices | Refrigeration Systems | Storage Displays | Bakery Ingredients
Oil Seeds | Agro Commodities | Tea | Milk | Diapers | Rice

INTERPLAST-PACK 2024
INTL TRADE EXHIBITION ON PLASTICS, POLYMERS, RUBBER, CORRUGATED PACKAGING & PRINTING

Products on Display:
Paper | Disposable Packaging Machinery | Plastic Raw Material
Polypropylene | Woven Products

Date & Venue
26-28 January 2024
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania

Timing
10:00 AM TO 6:00 PM

For more info, Please Call
0768 616 418 / 0656 482 557

## Wamiminika kuandika mahitaji baada ya Rais kumsaidia mmoja

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuahidi kumsaidia dada mmoja aliyemwomba cherehani kupitia akaunti yake ya Instagram, watu wameminika kwenye ukurasa huo nao wakiomba kusaidiwa.

Wako ambao waliomba fedha, bajaji, mitaji na wengine misaada ya maendeleo kwenye maeneo yao.

Pia ombi la kusaidiwa kutatua tatizo la kukatika umeme na kupanda kwa bei ya sukari, havikusahaulika kwa wafuatiliaji hao kwenye akaunti ya Rais.

Maombi yote hayo yaliandikwa Januari 24, mwaka huu, baada ya Rais Samia kuandika ujumbe akiwa nchini Indonesia kwa ziara ya kikazi.

Rais Samia aliandika: "Nimewasili nchini Indonesia kwa ziara ya kitaifa ya siku tatu, kufuatia (kutokana na) mwaliko wa kaka yangu, Mheshimiwa Rais Joko Widodo. Uhusiano wa Tanzania na Indonesia ambao mapema mwezi huu, (Januari 13), ulitimiza miaka 59.

"Umekuwa wenye tija kwa nchi yetu na mamilioni ya Watanzania hasa kwenye kilimo na biashara.Tunaendelea kuifanya kazi ya kukuza uhusiano huu ili kuleta tija zaidi kiuchumi kwa nchi yetu," aliandika Rais Samia

Baada ya Rais kuandika ujumbe huo, wengi walijitokeza kutoa maoni yao ikiwamo kumtakia kazi njema katika ziara yake hiyo, akiwamo dada ambaye jina lake lilisomeka Beatrice_only1, ambaye aliandika: "Sawa mama. Ukiwa unarudi nyumbani naomba uniletee zawadi ya cherehani."

Baada ya Beatrice kuandika ujumbe huo, Rais Samia naye alimjibu akisema: "Hujambo Beatrice? Nimepata wasaa wa kuusoma ujumbe wako. Hongera kwa kazi na kujituma. Wasaidizi wangu watawasiliana na wewe kukusaidia upate mashine uliyoomba kwa shughuli zako. Nakutakia kila la kheri."

Baada ya ujumbe huo wa Rais, watu wengine walijitokeza kuomba msaada, akiwamo aliyesomeka kwa jina la Emmanuel Joseph _tz, ambaye aliandika: "Mama mimi naomba mtaji nifanye biashara lakini nikifanikiwa nitakurudishia. Samahani wewe ndio mama yetu."

"@samia _suluhu_hassan, mama na mimi naomba unisaidie nipate walau timu ya kunifanyia majaribio, nina kipaji kikubwa cha soka," aliandika Nathan Ellyis.

Montana_outfits_backup aliandika: "Sawa mama. Ukiwa unarudi nyumbani naomba zawadi mama, pesa kidogo nifanye biashara yeyote ile mama." Mwingine, aliyesomeka Passionkid, aliandika: "Mama@Samia_Suluhu_Hassan, shikamoo. Ukirudi nyumbani naomba uniletee bajaji kwa ajili ya kupambana ili niweze kujikimu binafsi. Kingine nakutakia maisha marefu katika maendeleo katika nchi, nakupenda sana mama."

Official nadrio naye aliandika: "Mama naomba ajira hata ya kufagia Ikulu...mama yangu mimi ni Mtanzania halali."

"Mama tunakuomba ili suala la umeme limekua kero kubwa sana kwa wananchi wako. Kila siku kukatiwa umeme, biashara haziendi hata majumbani pia kukaa imekua adha kubwa,"aliandika hivyo Fabolously.

"Mama ukirudi naomba mtaji kidogo kwenye biashara yangu maana ni ndogo," aliandika Minah.cake.

Naye Geoorge Said aliandika; "Mama tunakuomba huduma za kiafya ziko gali sana mpaka kwa watoto wachanga, hii hali mjini je vijijini inakuwaje, wewe ndio msemaji wa mwisho."

Bishop Michale493 yeye aliandika: "Sisi tunaomba mama bei ya sukari ishuke tunauziwa elfu tano sukari kwa kilo, walala hoi tunauziwa bei sawa na Waziri anayonunua."

## HABARI KITAIFA

# Rais Samia ataja sababu tano kuwaleta wawekezaji Tanzania

**Na Gwamaka Alipipi,** INDONESIA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja sababu tano inazojivunia Tanzania kuwavutia wawekezaji kutoka Indonesia kuja kufanya uwekezaji nchini.

Alizitaja sababu hizo ni hali ya amani na usalama, mazingira mazuri ya kufanya biashara, ubora wa miundombinu, sera nzuri za uwekezaji pamoja na utawala thabiti wa uchumi wa nchi.

Alizitaja sababu hizo jana nchini Indonesia wakati akihutubia Jukwaa la Uwekezaji na Biashara, lililowakutanisha wafanyabiashara kutoka Tanzania na Indonesia.

Rais Samia alisema Tanzania inapakana na nchi nane ambazo inashirikiana nazo katika matumizi ya miundombinu ya barabara ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Malawi, Rwanda, Zambia na Rwanda.

Alisema hatua hiyo inawezesha wawekezaji kusafirisha na kuuza kwa urahisi bidhaa zao wanazozalisha wakiwa Tanzania kwenda katika nchi hizo.

"Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Hivyo ni mojawapo ya fursa kwa mwekezaji yeyote kuja kuwekeza Tanzania kwa sababu ataweza kuuza bidhaa zake katika nchi za jumuiya hizo zenye idadi ya watu zaidi ya mamilioni," alisema Rais Samia.

Kuhusu mazingira rafiki ya kufanya biashara, Rais Samia alisema Tanzania ina mazingira mazuri ya kumwezesha mwekezaji yeyote kuja kuwekeza.

Alisema ubora wa miundombinu husani usafiri wa barabara, reli na anga ni mojawapo ya sababu ya kuwavutia wawekezaji kuwekeza nchini.

Pia, Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye sera nzuri za uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na wawekezaji wanapokuja wanakutana na sheria rafiki pamoja na mazingira bora ya uwekezaji.

"Kuja kuwekeza Tanzania ni chaguo lilio jema, karibuni mje kuwekeza. Tanzania kuna mazingira bora na wezeshi ya uwekezaji kuliko nchi yoyote Afrika. Tanzania ni nchi ya ahadi katika uwekezaji, ukija hutajutia," alisema Rais Samia.

Aliuagiza uongozi wa TIC kuongeza kiasi cha ufanyaji biashara kati ya Tanzania na Indonesia kufikia Dola za Marekani bilioni moja katika miaka ijayo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, alisema wamesikia maelezo ya Rais na wanakwenda kutekeleza katika miaka mitano ijayo kutoka sasa.

Alisema Indonesia ni miongoni mwa nchi 19 duniani zenye uwekezaji mkubwa, yenye idadi ya watu zaidi ya milioni 250.

Teri alisema Tanzania husafirisha bidhaa mbalimbali kwenda Indonesia, ikiwamo korosho na karafuu na kununua mafuta ya kula kutoka nchini humo.

"Jiji la Jakarta ni eneo muhimu la uwekezaji, hivyo tulishakutana na wafanyabiashara kutoka hapa (Indonesia) na kuwashawishi waje Tanzania kuwekeza katika sekta ya kilimo, madini, nishati, utalii na usafirishaji," alisema.

# Anayedaiwa kinara mtandao dawa za kulevya mbaroni

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imemkamata kinara wa mtandao wa wafanyabiashara wa dawa hizo aina ya cocaine pamoja na jumla ya gramu 692.336 za Cocaine zinazowahusisha watuhumiwa wanne.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kamishna Mkuu wa DCEA, Aretas Lyimo, alisema mfanyabiashara huyo aliyekuwa akitafutwa kwa zaidi ya miaka 13 (jina limehifadhiwa), alikamatwa Boko, Dar es Salaam na washirika wake watatu ambao kati yao mmoja alikamatwa katika Kijiji cha Shamwengo, mkoani Mbeya.

Alisema mamlaka imebaini kuwa, wafanyabiashara wa matandao wa Cocaine husafirisha dawa hizo kwa kutumia watu wanaozimeza tumboni zaidi ya gramu 300 hadi 2,000 au kuweka kwenye maungo mengine ya mwili na mfanyabiashara huyo ana uwezo wa kusafirisha watu hadi 10 kwa siku kwenda mataifa mbalimbali.

"Mfanyabiashara aliyekamatwa ana mtandao mkubwa wa wabebaji maarufu (punda) kutoka nchi mbalimbali ambao huwatumia kusafirisha dawa hizo kwa njia ya kumeza. Makosa yake yanaangukia katika uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka," alisema na kuongeza:

"Mamlaka itafanya operesheni kali ya nchi kavu na baharini kwa mwaka huu, za nchi kavu zitahusisha mashamba ya dawa za kulevya, kwenye mipaka, maeneo ya mijini kwenye vijiwe vya usambazaji na watumiaji wa dawa za kulevya," alisema Lyimo.

Aidha, baharini operesheni zitahusisha fukwe na katikati ya bahari, na nyingine zitatekelezwa maeneo yote wanayouza shisha ili kubaini matumizi ya dawa za kulevya, akisisitiza wote watakaobainika kutumia dawa za kulevya kupitia shisha watachukuliwa hatua kali kisheria.

Operasheni hiyo itahusisha wauzaji wanaokiuka taratibu za uuzaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya na kemikali bashirifu.

Alitoa onyo kwa wote watakaoendelea kujihusisha na uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini kuacha kwa kuwa serikali imewezesha mamlaka kuwa na vifaa vya kisasa na mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea weledi kutekeleza operasheni hizo kwa ufanisi.

"Kwa wale wote watakaoendelea na kilimo cha bangi, mirungi na biashara ya dawa za kulevya za viwandani watashughulikiwa ipasavyo. Mamlaka inawaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za watu wote wanaojihusisha na biashara za dawa za kulevya kwa kupiga 119 ili kuhakikisha nchi inakuwa salama," alisema Lyimo.

Vilevile, alibainisha kuwa kwa sasa mkoa unaoongoza kwa kilimo cha bangi ni Mbeya ukifuatiwa na Morogoro, na kwa upande wa mirungi ni Kilimanjaro.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi yenye makao yake makuu Morogoro. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Wiki Kumi (10)<br>15/04/2024 – 22/06/2024 | Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya) |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**
Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads): Washiriki watajifunza mada mbali mbali kuhusu mbinu za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, watajifunza mada mtambuka ambazo zitahusu utaratibu wa namna ya kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara pamoja na Usimamizi wa kazi za Barabara.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hii yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za Udongo/Changarawe na Barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani **"SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS"** kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na **TARURA** au **TANROADS.**

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**
a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**
**Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo**

i. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi atalipa ada kiasi cha **Tsh. 1,600,000.**

Ada ya ushiriki ilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

S.L.P 963, MOROGORO.
Simu: 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957, MBEYA.
Simu: 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404/0765251509
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

# Tanzania, Indonesia zatia saini hati saba za ushirikiano

**Na Gwamaka Alipipi,** INDONESIA

ZIARA ya kitaifa ya siku tatu ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Indonesia imefanikisha kutiwa saini kwa hati saba za ushirikiano unaolenga kuboresha uwekezaji na biashara, sekta ya kilimo pamoja na elimu.

Vilevile, kuboresha sekta ya madini, uchumi wa buluu na masuala ya kidiplomasia baina ya mataifa hayo mawili.

Jana Rais Samia Suluhu Hassan na mwenyeji wake Rais wa Indonesia, Joko Widodo, walishuhudia kutiwa saini kwa hati hizo katika Ikulu ya Bogor, Indonesia.

Katika tukio hilo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, pamoja na Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutiwa saini kwa hati hizo, Rais Samia alisema Tanzania na Indonesia zina uhusiano wa muda mrefu na wa kihistoria ambao umetimiza miaka 60.

Alisema uhusiano huo uliasisiwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Rais wa Kwanza wa Indonesia, Sukarno.

Alisema Indonesia ilifungua ubalozi wake Tanzania mwaka 1964 na kuwa miongoni mwa nchi za kwanza kufungua ubalozi wake nchini miaka michache baada ya uhuru. Rais Samia alisema Tanzania ilifungua ubalozi wake nchini Indonesia Agosti, 2022.

Kuhusu ushirikiano katika kilimo, Rais Samia alisema Tanzania na Indonesia zimekubaliana kuboresha sekta ya kilimo hususani kuwapatia mafunzo mbalimbali wakulima yenye kuwaongezea uzalishaji.

"Tanzania na Indonesia zimekuwa zikishirikiana katika sekta ya kilimo, ambapo mwaka 1996 Indonesia ilianzisha kituo cha mafunzo ya kilimo kwa wakulima vijijini kilichopo Mikindo mkoani Morogoro. Kituo hicho kimekuwa kikitoa mafunzo kwa wakulima, hivyo ushirikiano wa leo unakwenda kuongeza undugu," alisema Rais Samia.

Kuhusu ushirikiano katika nishati Rais Samia alisema Indonesia imekubali kuja kufanya uwekezaji Tanzania hususani katika nishati safi ya kupikia.

Rais wa Indonesia, Joko Widodo alisema kuingiwa kwa hati hizo za ushirikiano kutaongeza zaidi ushirikiano na undugu baina ya mataifa hayo mawili uliodumu kwa zaidi ya miaka 60.


Alisema hati za ushirikiano zilizosainiwa ikiwamo ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) na PT Perusahaan Perdagangan Indonesea kutafanikisha kuongeza usafirishaji na uingizaji wa bidhaa na malighafi baina ya mataifa hayo pamoja na uwezo wa kufanya biashara.

Rais Samia aliwasili katika Ikulu ya Bogor, jana asubuhi na kupigiwa mizinga 21, kisha alikagua gwaride pamoja na kupanda mti wa kumbukumbu katika Ikulu hiyo.

Ziara ya Rais Samia nchini Indonesia imefanyika ikiwa imepita miezi mitano tangu Rais Widodo kufanya ziara ya kikazi nchini Tanzania.

Ushirikiano baina ya mataifa hayo mawili umeiwezesha Tanzania kuuza bidhaa mbalimbali nchini Indonesia ikiwamo pamba, tumbaku, karanga, kakao, matunda, kahawa, chai, njugumawe, mbegu za mafuta.

Bidhaa nyingine zingine ni za kilimo kama mafuta ghafi na mafuta ya mawese pamoja na sabuni. Katika sekta ya uwekezaji nchi ya Indonesia imewekeza Tanzania miradi mitano yenye thamani ya Sh. bilioni 6.5 sekta za kilimo, uzalishaji wa viwandani na ujenzi.



Mmiliki wa Kituo cha Mafuta cha Victoria, Harold Matemba (katikati), akipokea cheti cha uwakala wa uuzaji wa vilainishi vya Castrol Oil nchini kutoka kwa Meneja wa Castrol Oil Afrika Mashariki, Ed Savage, katika hafla iliyofanyika Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja wa Castrol Oil Tanzania, Omary Omary. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TARURA yahitaji bil. 3/- kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mvua

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Manispaa ya Morogoro inahitaji Sh. bilioni 2.9, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya madaraja na barabara zilizoharibiwa na mafuriko ya athari ya mvua inayoendelea kunyesha katika Manispaa na Wilaya ya Morogoro.

Meneja wa TARURA Manispaa ya Morogoro, Mhandisi Mohamed Muanda, alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari kuhusu ukaratabi wa miundombinu iliyoharibiwa na mvua.

Alisema wamefanya tathmini ya uharibifu wa miundombinu kwa ajili ya mvua zinazondelea kunyesha na kubaini kutokea uharibifu mkubwa ambao wanategemea fedha za kutoka serikalini na uharibifu mdogo ambao wana uwezo wa kuufanyia kazi.

Kadhalika, TARURA ina uwezo wa kukarabati miundombinu michache yenye kutumia gharama ndogo katika barabara nne kwa Manispaa kati ya barabara 44 zilizoharibika na Morogoro Vijijini kukarabati barabara moja kati ya tano zilizoharibika.

Alisema gharama za ukarabati mkubwa katika miundombinu ya barabara na madaraja kwa Manispaa ya Morogoro ni Shilingi bilioni mbili huku wilayani Morogoro ikihitajika Sh. milioni 900.

Mhandisi Maunda alisema miundombinu inayohitaji fedha nyingi ni pamoja na madaraja matano wilayani Morogoro ambayo ni Mto Kiroka- Bamba, Mkuyuni- Luhololе, Kiroka -Zahanati, Matuli Lilongwe na Sinyaulime na katika Manispaa ya Morogoro kuna madaraja mawili, Mzambarauni - Lukobe na Zahanati- Lukobe.

Alisema kukatika kwa madaraja na kuharibika zaidi kwa barabara hizo kumesababisha kukatisha mawasilino kwa wakazi wa maeneo hayo, ikiwamo kusimamisha shughuli za maendeleo.

Hata hivyo, alisema wanaendelea na ukarabati wa miundombinu ya barabara za ndani ya manispaa kwa kutumia wakandarasi waliopo licha ya mvua kuendelea kunyesha katika kila mkoa hapa nchini.

Aliwaasa wananchi kufuata maelekezo wanayopewa, ikiwamo kutopita kwenye barabara zinazojaa maji kwa kuhisi wanaweza kuvuka bali wasubiri hadi maji yapungue na waone barabara za kupita ili kuepusha ajali.

Aliwaomba wakazi wa Kata ya Mwembesongo kunakoendelea ujenzi wa barabara kuwa wavumivu hasa pale wanapokabiliwa na changamoto za uharibifu wa miundombinu ya maji na umeme hadi pale ujenzi utakapokamilika.

# TWCC yawasaidia wanawake kufikia soko huru la Afrika

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WATAALAMU wa taasisi zinazohudumia wajasiriamali wanawake mkoani Morogoro kupitia ofisi za Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), wanapaswa kuunda timu ndogo itakayosaidia kinamama kufikia soko huru la Afrika linalohudumia nchi 54 mapema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, Katibu Tawala Msaidizi upande wa biashara, viwanda na uwekezaji mkoani hapa, Beatrice Njawa, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya wajasiriamali wanawake kuhusu kanuni, taratibu na sheria za kufanyabiashara kwenye soko la Afrika (AICFTA), yaliyoandaliwa na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), ulifanyika mjini hapa.

Njawa alisema kwa kutumia taasisi mbalimbali kama Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), mkoa una kiu ya kuona wanawake wa Morogoro wanafikia nchi 54 kibiashara na kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Alisema anaamini wanawake waliopata mafunzo hayo watayatumia ipasavyo kama fursa kwa kujua masoko ya bidhaa wanazozalisha.

"Nipende kuwashukuru TWCC kwa kuandaa mafunzo haya kwa wanawake, fursa hii itawawezesha kujua masoko ya bidhaa mbali mbali ikiwamo ya Afrika Mashariki, hasa kwa kuzingatia ukuaji wa viwanda unaotegemea upatikanaji wa malighafi na masoko na kutumia soko huru la nchi 54 lilizopo kwa sasa," alisema.

Alisema mkoa umeandaa mpango wa kuwatambua wazalishaji wadogo na kuwasaidia katika urasimishaji bidhaa jambo ambalo ni changamoto kwao na kuwawezesha kufikia masoko ya nje kwa kufikia viwango vya kimataifa.

Makamu Mwenyekiti wa TWCC Taifa, Rose Romanus, alisema kwa sasa mazingira yamekuwa rafiki kwa biashara na kwamba mtu akijituma ana nafasi ya kufikia masoko yaliyopo na ndio maana wanafundisha kurasimisha baada ya kutengeneza bidhaa zinazokidhi viwango na kwenda kwenye soko la Afrika ambalo ni huru.

Alisema Mkoa wa Morogoro kama ulivyoongoza kwenye mashindano ya Jua Kali unapaswa kuendelea kuitendea haki kwa kuzingatia mafunzo hayo na kujiimarisha kwenye biashara zao.

Mmoja wa Washiriki, Hadija Mohamed, aliishukuru serikali kwa kuwakumbuka kwenye mambo mbalimbali huku akiwakumbusha kuwasaidia katika mitaji itakayowasaidia kukuza biashara zao na kufikia wateja wao kwa wakati.

"Tumeshaahidiwa mara nyingi kama tutapewa mitaji, lakini mpaka sasa ni kimya, tukipewa mitaji itatusaidia kukuza biashara hata kufikia viwango kwa masoko ya nje," alisema.

## Old Mutual yauza hisa zake UAP

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya kimataifa ya Old Mutual Limited jana ilitangaza kuuza hisa zake zote za biashara ya muda mfupi ya bima kwenye kampuni ya bima ya UAP Insurance Tanzania, kwa kikundi cha wanahisa wenye hisa chache. Mauzo ya hisa hizo yatakuwa rasmi baada ya kuidhinishwa na mamlaka za udhibiti wa bima nchini.

Uamuzi huo unatokana na mapitio ya kina ya kimkakati ya biashara kwa kuzingatia malengo ya muda mfupi na ya muda mrefu ya kampuni ya Old Mutual.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Old Mutual Holdings, Arthur Oginga, alisema: "Tangu tuinunue UAP Insurance Tanzania mwaka 2015, imekuwa ni dhamira yetu kukuza biashara kwa lengo la kuifanya kampuni hiyo iwe miongoni mwa watoa huduma za kifedha wanaoongoza kwenye soko la huduma hizo nchini Tanzania. Katika kutekeleza hilo tulifanya uwekezaji wa kimkakati ili kuhakikisha kuwa biashara yetu inabaki kwenye msingi imara na kushindana kwa mafanikio. Hata hivyo, biashara nchini Tanzania imekabiliwa na changamoto katika kurudisha mtaji kutokana na sababu mbali mbali za kiutendaji na kimazingira....," alisema.

Alisema wanatathmini mikakati mbalimbali ya kupata uongozi wa soko nchini Tanzania, lakini hawaoni njia ya kufikia lengo hilo la kimkakati. "Tathmini yetu imeonesha kwamba tutahitaji kufanya uwekezaji mkubwa zaidi ili kufikia malengo ya uongozi wa soko. Kutokana na hali hiyo, tumeamua kuuza hisa zetu kwa Strategic Ventures Company Limited, muungano kutoka kwa wanahisa wachache wa UAP Insurance Tanzania Limited."

UAP Insurance Tanzania imesema huduma na mahusiano na wateja na wadau wake nchini Tanzania vitabaki vilevile na itashirikiana na wamiliki wanaoingia ili kuendeleza huduma thabiti kwa wateja.

"Tunatumia fursa hii kuwataarifu wateja wetu na wadau wetu kwamba watarajie kuendelea kupata huduma bora zaidi."

Uwekezaji wa Old Mutual kwenye ukanda wa Afrika Mashariki bado ni thabiti. Hata hivyo, ukuaji huu unahitaji kuwa endelevu, kwa maslahi mapana ya wadau."

"Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, tuliamua kutumia jina la Old Mutual ili kuimarisha chapa yetu hapa Afrika Mashariki. Katika mwaka ujao, zoezi hili litaendelea, na tutaimarisha uwekezaji wetu ili kukuza biashara na kuendelea kuwa bora katika huduma jumuishi za kifedha," aliongeza Oginga.

"Tunawashukuru Watanzania kwa kutumia huduma za UAP Insurance na kampuni ya Old Mutual. Tunajivunia sana biashara ambayo tumeweza kuijenga nchini na kwa ufanisi wa timu yetu."



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso akizungumza na wakazi wa Murieti, jijini Arusha jana, alipofika kukagua maji yanayotoka kwenye mabomba katika eneo hilo, baada ya wakazi hao kulalamika kuwa wanapata maji ya chumvi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Miamala ya simu yaongezeka asilimia 30

**Na Restuta James**

MIAMALA ya kifedha kupitia simu za mkononi imeongezeka kwa asilimia 30 mwaka jana huku takwimu zikionesha kuwa Disemba watu walituma na kupokea Sh. 549,529,470.

Aidha, laini 30,309 zilifungiwa Disemba mwaka jana ukilinganisha na 34,848 zilizofungiwa Septemba 2023, ikiwa ni njia ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya Mawasiliano vyenye ubora kwenye soko.

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, kwa vyombo vya habari jana ilisema kwa robo ya mwisho ya mwaka jana, miamala iliongezeka kwa asilimia 44.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uwiano wa mawasiliano ya simu kwa idadi ya watu umeongezeka na simu za ulaghai zimepungua kati ya Januari na Desemba, 2023.

"Septemba, 2023 akaunti za pesa kwa simu zilikuwa 51,369,347 ambazo zilifanya miamala ya Sh. 422,390,546 na Desemba, 2023 zilifikia 52,875,129 zilizofanya miamala ya Sh. 549,529,470. Miamala ya Sh. 380,561,622 ilifanywa kupitia akaunti 42,120,445 Januari mwaka jana.

"Hali hii inaakisi kukua mfumo jumuishi wa kifedha nchini, huku mipango ikikamilika kuhakikisha huduma za mawasiliano zinafika sehemu nyingi," alisema Dk. Jabiri katika taarifa hiyo.

Kuhusu huduma za utangazaji, taarifa hiyo ilieleza kuwa mikakati imekamilika kutatua changamoto ya huduma za utangazaji wa redio kutofika baadhi ya sehemu nchini zenye hali ya mazingira magumu kijiografia, hasa zilizo pembezoni na maeneo yenye milima na mabonde.

Dk. Bakari alisema TCRA imeainisha maeneo yenye huduma hafifu na yasiyo na huduma za mawasiliano ya simu na intaneti baada ya kufanya utafiti nchini kote.

"Mamlaka imeendelea kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), juu ya uwezekano wa kujenga miundombinu mipya kwenye maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara kwa wawekezaji na ambayo hayajafikiwa na huduma ipasavyo," iliongeza taarifa hiyo.

Hata hivyo, alisema dakika za simu za kimataifa zinazoingia nchini zimeongezeka kwa asilimia 29.2; kutoka 2,216,904 Septemba 2023 hadi 3,129,711 Disemba 2023.

"Simu zenye uwezo mkubwa au simu janja, zimeenea kwa asilimia 32 miongoni mwa watu. TCRA itafuatilia kwa kina gharama za simu janja kwani kutokuenea kwa simu janja kwa watumiaji wengi ni mojawapo ya sababu za kutokuenea kwa matumizi ya intaneti kwa kasi," ilifafanua taarifa.

Taarifa hiyo imebainisha kwamba Tanzania imepata masafa mapya yatakayowezesha huduma ya intaneti ya kasi (5G), ambayo ni muhimu katika kuchochea uchumi wa kidijitali. Masafa hayo yalitolewa kwenye mkutano wa masuala ya masafa wa Desemba mwaka jana ulioandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Tanzania pia ilipata nafasi katika obiti ya satelaiti kwa ajili ya utangazaji; mafanikio yatakayowezesha kuenea huduma za utangazaji hasa kwenye maeneo yasiyo na usikivu mzuri wa redio yaliyopo pembezoni mwa nchi na yaliyozungukwa na milima ambapo matangazo ya mfumo wa utangazaji wa FM hayafiki.

Mawimbi ya FM yana changamoto ya kutofikisha matangazo mabondeni na sehemu zilizokingwa na milima ambapo watu wanaishi kama vile maeneo ya Rombo mkoani Kilimanjaro na kwingineko.

Taarifa hiyo imeeleza kwamba maeneo kumi (10) yenye changamoto hizo yametambulika baada ya utafiti na uchambuzi wa pamoja wa TCRA na UCSAF na yanategemewa kutengewa fedha kupitia utaratibu maalumu uliowekwa na mfuko huo.

# Wanakijiji wasusia kuzika maiti ifanyiwe uchunguzi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKAZI wa Kijiji cha Kisangiro kilichopo Kata ya Kirangi Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, wamegoma kuzika mwili wa kijana wao, Tefas Philipo (22) kuishinikiza Serikali kufanya uchunguzi baada ya kudai ameuawa kwa kuchomwa na mshale wenye sumu na jamii ya wafugaji wa Kimasai.

Inadaiwa Januari 8, mwaka huu,Tefasi alishambuliwa kwa kuchomwa na mshale huo na kundi la vijana 40 wafugaji hao akiwa shambani na wenzake wakifanya usafi na kufa wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Akizungumzia tukio hilo nje ya chumba cha kuhifadhia maiti cha Mount Meru, Diwani wa Kata ya Kirangi, Philipo Moloi, alisema Januari 17, mwaka huu, Tefasi alifariki dunia hospitalini hapo.

Moloi alisema tukio hilo limetokea wakati kukiwa na mgogoro wa ardhi uliodumu kwa zaidi ya miaka 30 kati ya Kijiji cha Kisangiro na Naan vilivyopo wilayani humo.

"Hatuchukui mwili mpaka Serikali itakapoufanyia uchunguzi pamoja na kutoa tamko kuhusu mgogoro wa ardhi na kuuawa kwa kijana wetu," alisema.

Alisema tangu mwaka 1993 mgogoro huo ulipoanza kumeundwa tume mbalimbali kutatua mgogoro huo lakini zimeshindwa kupata suluhu.

"Januari 8 ,mwaka huu, vijana wetu wakiwa shambani wakifanya usafi walishambuliwa na kikundi cha watu zaidi 40 na katika hali ya kujinasua watano walijeruhiwa, lakini wanaendelea vizuri kwa kuwa wamepatiwa matibabu katika vituo vya afya na zahanati, mmoja amefariki baada ya kupatiwa rufani ya kuja kutibiwa hapa Mount Meru kwa kuwa alichomwa na mshale wenye sumu.

"Tunaiomba Serikali kuhakikisha inatatua mgogoro huu kwa kuwa tunapoteza nguvu kazi ya taifa kwenye kijiji chetu, hatuwezi kuishi kwa namna hii," alisema. Mwenyekiti wa Kijiji cha Kisangiro, Wikasi Guruma, alisema wamekuwa na matatizo ndani ya kijiji hicho mgogoro huo ambao umedumu kwa muda mrefu bila ya kupatikana kwa ufumbuzi, unaendelea kutishia maisha yao.

"Kijana wetu alikuwa shambani akisafisha shamba, ghafla alivamiwa na kundi la vijana 40 wenye mishale, katika harakati za kujitetea alijeruhiwa na baadaye alifariki," alisema.

Kaka wa marehemu huyo, Simon Phillipo, alisema walikutwa shambani wakifanya kazi na kuzungirwa na kundi hilo na kushambuliwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo amethibisha kutokea mapigano hayo na kwamba wiki mbili zilizopita walikwenda kwenye eneo hilo wakiambatana na viongozi wa Wilaya ya Ngorongoro na kuweka mambo sawa.

"Kuhusu suala la mtu kufariki ngoja nifuatilie, lakini kuhusu mapigano timu ilikwenda na kutatua kero hiyo kwa kuwa walikuwa wanagombea mpaka uliowekwa na Serikali," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuna jambo la kujifunza kuhusu uhaba wa sukari

**KILA** kona sasa ni kilio. Ndivyo ilivyo katika nchi kutokana na kuadimika kwa sukari kwenye soko nchini na pale inapopatikana bei yake haishikiki. Katika baadhi ya maeneo, bidhaa hiyo muhimu kwa matumizi ya kila siku inauzwa kati ya Sh. 5,000 na 6,000 kwa kilo.

Suala la kuadimika kwa bidhaa hiyo ambayo hutumika kwa masuala mbalimbali yakiwamo kifungua kinywa, na kutengeneza vyakula na vinywaji, lilianza kama mzaha lakini sasa limekuwa sugu. Kuwapo kwa tatizo hilo ni tofauti na ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa na serikali kwamba upungufu wa sukari utakuwa historia baada ya Kampuni ya Sukari ya Bagamoyo na Kiwanda cha Mkulazi mkoani Morogoro kukamilika.

Katika miaka kadhaa iliyopita, bidhaa hiyo iliadimika katika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha serikali, chini ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kufanya msako katika maghala ya wafanyabiashara na kukamata tani nyingi zikiwa zimefichwa. Pamoja na kupatikana katika maghala, sababu nyingine iliyotolewa ni kwamba baadhi ya viwanda vinavyozalisha bidhaa vilikuwa vimefungwa kwa ajili ya ukarabati ikiwa ni maandalizi ya uzalishaji katika msimu mpya unaofuata.

Aidha, serikali ilitoa tamko kwamba pamoja na kuadimika na kufungwa kwa viwanda kama ilivyoelezwa na wamiliki, kiwango kinachozalishwa nchini ni kidogo kulinganisha na mahitaji halisi katika soko.

Kutokana na sababu hiyo, ilielezwa kuwa serikali inatafuta suluhisho la kudumu la kuhakikisha sukari inapatikana kwa ajili ya kutosheleza soko la ndani pamoja na kuwapo kwa ziada ambayo itasaidia kupunguza makali pindi kunapokuwa na upungufu.

Miongoni mwa mipango iliyobainishwa na serikali ni upanuzi wa viwanda vilivyokuwapo kwa wakati huo vya Kilombero, Kagera, Mtibwa na Kilimanjaro (TPC). Pia iliweka bayana kuwa ujenzi wa viwanda vya Bagamoyo na Mkulazi pia vitakapoanza uzalishaji vitapunguza tatizo, hivyo wananchi kupata bidhaa kwa urahisi na kwa bei nafuu. Licha ya kiwanda cha Bagamoyo ambacho kinamilikiwa na kundi la Kampuni za Bakhresa kuanza uzalishaji na Mkulazi kikiwa katika hatua za mwisho za kuanza uzalishaji, uhaba wa sukari umekuwa mkubwa zaidi na kuwa anasa kwa wananchi wa kawaida kutokana na bei yake kupaa maradufu.

Kuwapo kwa hali hii kunaibua maswali mengi ambayo baadhi yanakosa majibu ya moja kwa moja na matokeo yake wananchi wengi wanaumia ama kwa kukosa sukari au kushindwa kumudu bei iliyoko sokoni kwa sasa. Mbali na hiyo, hivi sasa katika maeneo mengi, mkoa wa Dar es Salaam ukiwamo, bidhaa hiyo haipatikani. Katika siku mbili zilizopita, wananchi wamekuwa wakiisaka bidhaa hiyo madukani, kutoka duka moja hadi lingine, huku majibu wanayopewa ni kwamba haipo.

Suala la viwanda kukarabatiwa ni la kila mwaka na sukari imekuwa ikipatikana na kama ni kwa upungufu si kama wa mwaka huu. Jambo la kujiuliza ni je, Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) na Wizara ya Kilimo hawajui kama kuna uwezekano wa kuwapo kwa upungufu au kuadimika kwa bidhaa hii? Kama wanajua ni hatua gani wamechukua ili kuhakikisha wananchi hawapati adha kama ilivyo sasa?

Pamoja na kuwapo kwa maswali hayo ambayo ni vigumu kupata majibu, jambo la faraja ni kwamba serikali kupitia Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, imetamka kuwa tatizo hilo linatarajiwa kumalizika ifikapo Februari 15, mwaka huu. Amesema kumalizika kwa tatizo hilo kunatokana na kutoa vibali vya kuagiza kutoka nje.

Kuna msemo kwamba kila siku binadamu anajifunza kutokana na makosa au uhalisia wa mambo katika maisha ya kila siku. Ni vyema funzo likatolewa na kupata mbinu za kutatua tatizo hilo pindi litakapojitokeza siku zijazo badala ya kuacha wananchi wakaumia mara kwa mara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Madereva wa bodaboda, bajaji vituo vyao viepushe usumbufu

**BIASHARA** ya bodaboda na bajaj, imehalalishwa tangu serikali iliporuhusu usafiri huo miaka mingi iliyopita na kutungiwa kanuni mwaka 2010.

Hata hivyo, licha ya kuhalalishwa kwa usafiri huo, bado kuna changamoto mbalimbali inayowakabili madereva wa vyombo hivyo vya moto.

Miongoni mwa changamoto hizo ni ukosefu wa vituo vyao vya kusubiria na kushusha hali ambayo inawafanya walazimike kujichanganya kwenye vituo vya daladala.

Mchanganyiko huo wa daladala, bodaboda na bajaj, unasababisha kuwapo msongamano mkubwa wa vyombo hivyo na kuleta usumbufu kwa abiria.

Kwa mfano, kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho Dar es Salaam, msongamano ni mkubwa unaokifanya kituo hicho kuonekana ni kidogo kutokana na mchanganyiko huo ambao pia unachagizwa na wafanyabiashara wadogo.

Ninadhani ipo haja kwa halmashauri kutenga vituo vya usafiri huo ili visichanganywe na vya daladala.

Ikumbukwe kuwa wakati mwingine madereva wa daladala na hao wa bodaboda na bajaj huwa wanapigana kugombea abiria.

Vitendo kama hivyo ni hatari kwa usalama wao. Ili kuondoa sintofahamu hiyo, ninadhani watengewe vituo vyao rasmi.

Hatua hiyo itasaidia hata wale wanaosubiri abiria katika maeneo hatarishi wawe katika vituo vyao na kuendelea na biashara bila usumbufu.

Usafiri wa bodaboda na bajaj umeajiri watu wengi wakiwamo wasomi na wasiosoma vidato, biashara hiyo inaendelea kukua kila uchao.

Hivyo, ninadhani ingesaidia kujua zaidi, hasa kwa kujengewa vituo, ili abiria wanaotaka kutumia usafiri wafuate ulipo badala ya kuchanganywa na daladala na kusababisha vurugu zisizo za lazima.

Pamoja na kwamba halmashuri zina jukumu la kuwatengea maegesho, lakini pia kuna ya kushirikisha wadau mbalimbali kufanikisha lengo. Ninaamini kwamba changamoto ya bodaboda na bajaj haiwezi kumalizwa na halmashauri na polisi tu, bali ni wadau wote wa sekta ya usafiri kushiriki kwa kutoa ushauri au maoni.

Kimsingi, unahitajika mkakati mpana na jumuishi kwa ajili ya kumaliza changamoto hiyo ya muda mrefu, kwani ni jambo la ajabu kuona usafiri huo umeruhusiwa halafu hakuna maeneo ya maegesho au vituo. Aidha, ni muhimu pia kuzingatia usafiri huo kwenye ubunifu wakati wa ujenzi wa barabara, ili nao wawe na njia za kupita badala ya kujichanganya na magari kitendo ambacho wakati mwingine husababisha wagongwe na magari.

Lakini pia ni vyema usafiri huo ukawa na njia zake maalum ambazo ni vyema zikahusianishwa na sheria ya Usalama Barabarani na za Usafirishaji kwa ujumla.

Vilele ni muhimu utaratibu huo ukawa na mfumo wa utambuzi wa bodaboda na bajaj na kuwekeza miundombinu ya usajili katika kila halmashauri na ngazi ya taifa.

Pamoja na hayo, kuna haja ya kuwekeza katika utoaji wa elimu ya usalama barabarani ili waweze kuzingatia na kuepusha ajali zisizo za lazima.

Madereva wengi wa vyombo hivyo kama si wote, wana tatizo la kutoheshimu sheria wawapo barabarani.

Imekuwa ni jambo la kawaida kukuta dereva wa bodaboda au bajaj kuvuka makutano ya barabara bila kusubiri kuruhusiwa na taa, kitendo ambacho ni hatari kwake na kwa abiria.

Madereva wa bodaboda wanaruhusiwa kubeba abiria mmoja, lakini wao wanabeba hata watatu, bajaj wanaruhusiwa kubeba abiria watatu, lakini wao wanabeba hata watano.

Kwa mifano hiyo, ni wazi kwamba kuna tatizo kwa upande wa kuheshimu sheria ya usalama barabarani, hivyo elimu inahitajika kwa wingi ili kunusuru maisha yao na ya abiria wao.

# Biteko: Watanzania wapewe kipaumbele mradi EACOP

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amewataka watendaji katika kampuni inayotekeleza Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kuhakikisha Watanzania wanapewa kipaumbele katika hatua zote za utekelezaji wa mradi ikiwamo ajira na utoaji huduma za ulinzi, chakula, usafiri, bidhaa za ujenzi, huduma za mawasiliano na nyingine ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Nishati ya mwaka 2015.

Dk. Biteko alisema hayo baada ya ziara katika Kata ya Chongoleani, jijini Tanga na kujionea kazi mbalimbali za ujenzi wa miundombinu zikiendelea katika eneo hilo ambalo mafuta kutoka nchini Uganda yatakuwa yakipokewa na kuhifadhiwa kabla ya kusafirishwa.

Katika ziara hiyo aliambatana na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

"Serikali inataka kuona Watanzania wengi zaidi wanapewa kipaumbele cha ajira katika hatua zote za mradi na hii inajumuisha kampuni za Watanzania zinazotoa huduma mbalimbali kwa kada ambazo ujuzi wake unapatikana ndani ya nchi, wapatiwe nafasi na kwa kada ambazo zinahitaji wataalam wa nje lazima kuwe na uwiano wa malipo kati ya wazawa na wageni," alisisitiza Dk. Biteko.

Kuhusu ujuzi unaotolewa na kampuni ya EACOP kwa Watanzania wakiwamo kutoka vijiji vinavyozunguka mradi, Dk. Biteko alitaka kampuni hiyo kutoa ujuzi endelevu utakaowawezesha kuendelea na kazi hata utakapokamilika akitoa mfano kuwawezesha kupata mashine za uchomeleaji na ametaka halmashauri zishirikiane na kampuni ili kutekeleza suala hilo.

Akizungumzia utekelezaji mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi litakalokuwa na urefu wa kilomita 1,443, alisema naendelea vizuri na sasa umefikia asilimia 32 na mabomba yatakayopitisha mafuta yanaendelea kuingia nchini kwa ajili ya kuwekewa mifumo ya upashaji joto na plastiki itakayozuia upotevu wa joto kwenye mabomba hayo katika kiwanda kilichopo Sojo, wilayani Nzega.

Alisema, ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha mkuza wa bomba umekamilika, kambi za ujenzi zimekamilika na kazi mbalimbali zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa gati katika kata ya Chongoleani, mkoani Tanga kwa kupakia mafuta na kusafirishwa nje ya nchi.

Alisema, serikali ina kiu ya kuwaletea maendeleo Watanzania na ikiamua kutekeleza jambo inafanya bila ulegevu na kwamba Tanzania imeshatoa zaidi Dola za Marekani milioni 240 EACOP kama mwanahisa ambaye ana asilimia 15 kwenye mradi huo na fedha hizo zinatolewa kwa wakati. Katika hatua nyingine, Dk. Biteko amekagua eneo la mafuta yanapopokeewa katika Bandari ya Tanga na kukagua mita za kupimia mafuta (flow meter) na aliridhika kuwa mita hizo zinafanya kazi vizuri na kuleta ufanisi katika shughuli za upakuaji na upakiaji mafuta katika Bandari ya Tanga.

Alisema, baada ya kurekebishwa kwa kanuni za mafuta, serikali imeshaagiza yote ya ukanda wa Kaskazini yachukuliwe jijini Tanga pamoja na yanayoenda nchi za nje kama Kenya na ya ukanda wa Kusini yachukuliwe Bandari ya Mtwara.

Aliziagiza taasisi zinazosimamia mafuta ikiwamo EWURA, PBPA, TBS na TPA, kufanyia kazi haraka agizo hilo la serikali kwa kuwa kanuni zilishasainiwa kwa ajili utekelezaji wa suala hilo ili kuwawezesha Watanzania kupata mafuta kwa bei nafuu.

Akiwa jijini Tanga, Dk. Biteko pia alitembelea eneo la hifadhi ya mafuta ya kampuni ya GBP ambayo inahifadhi mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi na kuwaeleza wawekezaji hao kuwa, serikali inathamini uwekezaji huo na ipo tayari kuwaunga mkono katika mipango yao ya uwekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka nguvu kubwa kwenye utekelezaji wa mradi huo, ambao utakuza pia mapato ya mkoa na kipato cha mtu mmoja mmoja.

# Machinga wadai makubaliano yamekiukwa

**Thomas Wandiba,** SAUT

BAADHI ya wafanyabiashara wadogo maarufu 'Machinga' katika soko la Mchafukuoga jijini Mwanza, wamelalamika kutotekelezwa kwa makubaliano waliyowekeana na serikali wakati wanahamishwa kutoka katika maeneo ya katikati ya mji hali inayoendelea kuwaumiza katika biashara zao.

Makubaliano hayo ni pamoja na kuwekewa miundombinu rafiki, kituo cha daladala pamoja na kukamilisha kwa wakati soko jipya la eneo hilo ambalo lilitakiwa liwe limekamilika, lakini mpaka sasa wanadai hawajaona matokeo.

Wafanyabiashara hao ambao wengi wao walitolewa katika eneo la Makoroboi, walibainisha hayo kwa nyakati tofauti sokoni hapo wakati wakizungumza na Nipashe na kubainisha kuwa kero hizo zimerudisha kwa kiasi kikubwa shughuli zao za kibiashara.

"Awali daladala zilianza kupita katika eneo hili, lakini kutokana na ubovu wa barabara zimeacha kabisa, hivyo hata wateja tuliozoea wakija huku kwajiili ya kununua bidhaa hawaji tena hali inayosababisha baadhi yetu kurudi katika maeneo tulipoondolewa," alisema mfanyabiashara Juma Kimaro.

Aliiomba serikali kutimiza ahadi walizozitoa kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki kwa biashara katika soko hilo ambalo linakumbwa na tatizo la maji kutuama na kutengeneza tope linalosababisha wateja kushindwa kuingia.

"Hapa linajengwa soko ambalo lilitakiwa kuwa limekamilika mpaka sasa, lakini hatuoni matokeo pengine lingetusaidia kuondoka katika tope hili, tunaomba serikali izuie minada katika maeneo nje ya masoko haya kwani inatukosesha wateja," alisema Ramadhani John mfanyabiashara. Mwenyekiti msaidizi wa soko hilo, Victoria Said, alikiri kuhitaji kituo cha daladala karibu na soko hilo kama walivyokubaliana na serikali kwa kuwa eneo tayari lipo ni utekelezaji waweze kupata wateja.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Nyamagana Mhandisi. Danstan Kishaka, alikiri kuwapo tatizo la ubovu wa barabara unaotokana na mvua inayoendelea kunyesha ambaye alisema tayari kazi hiyo ame-


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2023.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2023 | Robo Mwaka iliopita 30 Septemba 2023 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 511.52 | 315.63 |
| 2 | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 9,797.16 | 9,787.52 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za serikali | 38,180.41 | 37,814.22 |
| 4 | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,117.74 | 687.01 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22.94 | 25.99 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 3,517.44 | 3,989.91 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 46,772.72 | 47,709.24 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,514.82 | 1,974.01 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 888.92 | 863.40 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **102,323.67** | **103,166.91** |
| B | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,700.00 | 1,247.00 |
| 18 | Amana za Wateja | 56,379.50 | 58,280.42 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,836.95 | 1,726.46 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 785.47 | 675.05 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **60,701.92** | **61,928.94** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **41,621.75** | **41,237.98** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 261.30 | 190.10 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 7,386.41 | 7,457.61 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,144.04 | 760.27 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,621.75** | **41,237.98** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 4,305.11 | 6,738.45 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 349.31 | 120.32 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 178.13 | 153.61 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 40.68% | 39.97% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.74% | 0.25% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80.80% | 80.35% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 45.71% | 46.24% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87.55% | 87.43% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -2.43% | -4.10% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.82% | -2.13% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2023.

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2023 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31 Desemba 2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Desemba 2023 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Desemba 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,052.38 | 2,039.64 | 8,529.50 | 8,707.52 |
| 2 | Gharama za Riba | 661.77 | 722.79 | 2,985.09 | 3,258.97 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,390.61** | **1,316.85** | **5,544.41** | **5,448.54** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0.00 | 951.18 | 258.71 | 951.18 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 24.52 | 2.97 | 100.09 | 6.13 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **214.73** | **240.35** | **643.43** | **703.93** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 37.35 | 55.30 | 122.92 | 196.93 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 177.38 | 185.04 | 520.51 | 507.00 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,069.66** | **989.89** | **3,990.20** | **3,839.70** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 389.35 | 394.37 | 1,570.03 | 1,633.82 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 10.35 | 12.78 | 28.59 | 34.07 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 669.96 | 582.74 | 2,391.57 | 2,171.82 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **511.17** | **(386.84)** | **1,838.84** | **1,355.47** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 127.40 | (187.36) | 694.80 | 460.03 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **383.77** | **(199.48)** | **1,144.04** | **895.43** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 24 | 26 | 24 | 26 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 12 | (6) | 35 | 27 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 12 | (6) | 35 | 27 |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.53% | -0.77% | 1.09% | 0.76% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.70% | -1.95% | 2.78% | 2.19% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 66.63% | 63.57% | 64.48% | 62.41% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6.43% | 5.58% | 5.90% | 5.04% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2023.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2023 | Robo Mwaka iliopita 30 Septemba 2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Desemba 2023 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Desemba 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 383.77 | 345.23 | 1,144.04 | 895.43 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara katika mali | 100.23 | 96.05 | 388.28 | (21.89) |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | 936.51 | 3,127.45 | 3,272.45 | 1,070.21 |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | (1,447.92) | (2,547.98) | (5,239.23) | (29,765.88) |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 405.48 | 332.90 | 1,040.27 | 607.54 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 576.35 | (718.28) | (453.56) | 113.36 |
| | Kodi iliyolipwa | (127.40) | (127.40) | (694.80) | (460.03) |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **827.02** | **507.98** | **(542.56)** | **(27,561.25)** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | - | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (125.75) | (0.00) | (127.84) | (401.10) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (6,293.93) | 2,720.78 | (7.93) | (6,999.96) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(6,419.68)** | **2,720.78** | **(135.77)** | **(7,401.06)** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | (164.15) | (164.15) | (492.45) |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | (67.97) | (67.97) | (284.53) | 439.73 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(67.97)** | **(232.12)** | **(448.68)** | **(52.72)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (5,660.64) | 2,996.63 | (1,127.01) | (35,015.03) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 16,619.61 | 13,622.97 | 12,085.98 | 47,101.31 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **10,958.97** | **16,619.61** | **10,958.97** | **12,086.28** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 31/12/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,144.04 | - | - | - | **1,144.04** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (164.15) | - | - | - | **(164.15)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 206.39 | (206.39) | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **8,530.44** | **261.30** | **-** | **-** | **41,621.75** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **6,129.50** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 895.43 | - | - | - | **895.43** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (492.45) | - | - | - | **(492.45)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 811.68 | (811.68) | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2023**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 24-01-2024 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 24-01-2024 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 24-01-2024 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-01-2024 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-01-2024 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

Access Microfinance Bank Tanzania

## ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED**
**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2023**

| | | (Kiasi kwa shilingi milioni) | |
|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa<br>31 DISEMBA 2023 | Robo Mwaka iliopita<br>30 SEPTEMBA 2023 |
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 6,076 | 5,396 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 8,861 | 8,991 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 147 | 375 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 17 | 28 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 200 | 200 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 55,176 | 53,945 |
| 12 | Mali Nyingine | 7,570 | 7,592 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 666 | 729 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **78,713** | **77,256** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 500 | - |
| 18 | Amana za Wateja | 61,734 | 59,647 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 712 | 951 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,508 | 1,578 |
| 27 | Dhima Nyingine | 5,570 | 6,344 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **70,025** | **68,520** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **8,689** | **8,736** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (32,537) | (32,537) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,225 | 1,273 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,688** | **8,736** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 653 | 170 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 3,780 | 4,414 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,761 | 4,495 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.04% | 11.31% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.31% | 7.55% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 96.31% | 97.98% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 70.10% | 69.83% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70.35% | 70.09% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 4.34% | 3.14% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1.89% | 2.39% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2023**

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Mwaka sasa<br>31 DISEMBA 2023 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita)<br>31 DISEMBA 2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa<br>31 DISEMBA 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita)<br>31 DISEMBA 2022 |
| 1 Mapato ya Riba | 6,657 | 5,646 | 24,916 | 18,719 |
| 2 Gharama za Riba | (1,170) | (1,103) | (4,766) | (3,548) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 5,487 | 4,542 | 20,150 | 15,171 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,493) | (473) | (2,617) | (2,490) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,391** | **1,302** | **5,041** | **6,415** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 182 | 41 | 174 | 94 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 391 | 354 | 1,522 | 3,069 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 818 | 907 | 3,344 | 3,251 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,219)** | **(4,991)** | **(20,871)** | **(18,038)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,105) | (3,077) | (12,426) | (11,214) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (155) | (149) | (553) | (567) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (1,960) | (1,765) | (7,892) | (6,257) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **166** | **380** | **1,703** | **1,059** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (214) | (194) | (478) | (12) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(48)** | **186** | **1,225** | **1,047** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(48)** | **186** | **1,225** | **1,047** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 376 | 383 | 376 | 383 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (5) | 19 | 31 | 19 |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.25% | 1.07% | 1.62% | 1.15% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -2.21% | 10.39% | 14.68% | 11.14% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 64.85% | 71.84% | 69.67% | 71.73% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 39.80% | 38.65% | 38.31% | 38.72% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2023**

| | *(Kiasi kwa shilingi milioni)* | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa<br>31 DISEMBA 2023 | Robo Mwaka iliyopita<br>30 SEPTEMBA 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa<br>31 DISEMBA 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita)<br>31 DISEMBA 2022 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 166 | 452 | 1,703 | 1,059 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 1,893 | 764 | 4,287 | 1,760 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,724) | (1,070) | (9,898) | (10,295) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (19) | - | (19) | (7) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,587 | 1,817 | 8,806 | 10,715 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (892) | (291) | (1,312) | (765) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (431) | 964 | 777 | 216 |
| - Kodi Iliyolipwa | (55) | (75) | (595) | (218) |
| - Mengineyo (bainisha) | (88) | (219) | (452) | (583) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **437** | **2,342** | **3,298** | **1,882** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (43) | (57) | (300) | (196) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 19 | - | 25 | 8 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | (47) | (603) | (669) | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(71)** | **(660)** | **(944)** | **(188)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (143) | (204) | (874) | (993) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **(143)** | **(204)** | **(874)** | **(993)** |
| | | | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **223** | **1,478** | **1,480** | **702** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **11,534** | **10,056** | **10,277** | **9,575** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **11,757** | **11,534** | **11,757** | **10,277** |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2023**

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mtaji wa Hisa** | **Malipo juu ya bei ya hisa** | **Mapato Yaliyobakizwa** | **Ziada ya Kisheria** | **Tengo la Ziada ya Jumla** | **Jumla** |
| **Kipindi cha sasa hadi 31 Disemba 2023** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2023 | 40,000 | - | (32,537) | - | - | 7,463 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,225 | - | - | 1,225 |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2023** | **40,000** | **-** | **(31,312)** | **-** | **-** | **8,688** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 31 Disemba 2022** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2022 | 40,000 | - | (33,813) | 229 | - | 6,416 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,047 | - | - | 1,047 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 229 | (229) | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2022** | **40,000** | **-** | **(32,537)** | **-** | **-** | **7,463** |

## AADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2023

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zisizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Julius Justine Ruwaichi | Afisa Mtendaji Mkuu | Imesainiwa | 22 Januari 2024 |
| Tajinder Singh Bhachu | Mkuu wa Fedha | Imesainiwa | 22 Januari 2024 |
| Catherine Temu | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Imesainiwa | 22 Januari 2024 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| **Jina** | **Cheo** | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Thomas Engelhardt | Mwenyekiti | Imesainiwa | 22 Januari 2024 |
| Johannes Mainhardt | Mkurugenzi | Imesainiwa | 22 Januari 2024 |

Access Microfinance Bank Tanzania

## ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

# MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|
| **ACCESS RAHISI,NORMAL SAVINGS, RAHISI CAA, ELIMU, AND KIKUNDI ACCOUNT(RAHISI ACCOUNT)** | **TZS** | **USD** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | - |
| Monthly service fees | 2,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | - |
| Bank statement 1free per month | FREE | - |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | - |
| New ATM card issuance | 10,000.00 | - |
| ATM card renewal or replacement | 10,000.00 | - |
| Replacement of the PIN | 10,000.00 | - |
| Standing order Internal | 2,000.00 | - |
| Standing order External | 12,980.00 | - |
| Dormant account fee | FREE | - |
| **Interbank Transfer** | | - |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | - |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | - |
| >50,000,000 | 10,000.00 | - |
| International transfer | | Up to USD 55 |
| Closure of account | 10,000.00 | - |
| **NUFAIKA TRANSACTIONAL ACCOUNT** | | |
| Required minimum opening balance | 50,000.00 | 25.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| **Interbank transfer** | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | N/A | Up to USD 55 |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **NORMAL CURRENT ACCOUNT (NUFAIKA ACCOUNTS)** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | 0.18% |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | 10 |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement once free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | N/A |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| **Interbank transfer** | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **SPECIAL ACCESS NUFAIKA ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 60,000.00 | 50.00 |
| Minimum monthly turover | 20,000,000.00 | 10,000.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | 0.18% |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement once free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | N/A |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| **Interbank transfer** | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | N/A | 55.00 |
| Dormant account fee | 5,000.00 | 5.00 |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **MIKAKATI SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 20,000.00 | 20.00 |
| Monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 20,000.00 | 20.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | N/A | Up to USD 55 |
| Account closure | 12,000.00 | 5.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **MIKAKATI PLUS SAVING ACCOUNTS** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | 10,000.00 | | |
| Monthly service fees | | | FREE | | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | | |
| Cash withdrawal over counter | | | ONCE FREE PER MONTH | | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 5,000.00 | | |
| Dormant account fee | | | FREE | | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | 12,000.00 | | |
| **KIKUNDI SAVING ACCOUNT** | | | **TZS** | | |
| Required minimum opening balance | | | 10,000.00 | | |
| Monthly service fees | | | FREE | | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | | |
| Cash withdrawal over counter | | | 3,000.00 | | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 3,000 | | |
| Dormant account fee | | | FREE | | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | FREE | | |
| **BARAKA JUNIOR ACCOUNT** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | - | - | |
| monthly service fees | | | FREE | FREE | |
| Bank statement 1free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cash withdrawal over counter | | | FREE | FREE | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | FREE | FREE | |
| Dormant account fee | | | FREE | FREE | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | FREE | FREE | |
| **TERM DEPOSIT RATES 2023** | | | | | |
| **Amount** | | | **Interest Rates** | | |
| 5,000,000 - 500,000,000 | | | 3% - 12% p.a | | |
| > 500,000,000 | | | Negotiation | | |
| **AGENCY BANKING** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| **Withdrawal (TZS) (agents) Range** | **TZS** | | | | |
| 100-2999 | 10 | 710 | 450 | 350 | 810 |
| 3000-3999 | 14 | 711 | 450 | 350 | 814 |
| 4000-4999 | 27 | 719 | 450 | 350 | 827 |
| 5000-6999 | 54 | 739 | 450 | 350 | 854 |
| 7000-9999 | 56 | 770 | 450 | 350 | 856 |
| 10000-14999 | 102 | 788 | 450 | 350 | 902 |
| 15000-19999 | 195 | 924 | 450 | 350 | 995 |
| 20000-20000 | 306 | 1,127 | 450 | 350 | 1,106 |
| 20001-29999 | 306 | 1,372 | 1,400 | 700 | 2,406 |
| 30000-39999 | 351 | 2,672 | 1,400 | 700 | 2,451 |
| 40000-49999 | 419 | 2,770 | 1,400 | 700 | 2,519 |
| 50000-99999 | 573 | 3,050 | 1,400 | 700 | 2,673 |
| 100000-100000 | 707 | 3,435 | 1,400 | 700 | 2,807 |
| 100001-199999 | 707 | 3,771 | 2,620 | 980 | 4,307 |
| 200000-200000 | 821 | 5,271 | 2,620 | 980 | 4,421 |
| 200001-299999 | 821 | 5,558 | 3,325 | 1,275 | 5,421 |
| 300000-300000 | 838 | 6,558 | 3,325 | 1,275 | 5,438 |
| 300001-399999 | 838 | 6,950 | 3,950 | 1,650 | 6,438 |
| 400000-499999 | 982 | 7,950 | 3,950 | 1,650 | 6,582 |
| 500000-599999 | 1,245 | 8,370 | 3,950 | 1,650 | 6,845 |
| 600000-699999 | 1,532 | 9,140 | 3,950 | 1,650 | 7,132 |
| 700000-750000 | 1,700 | 9,980 | 3,950 | 1,650 | 7,300 |
| 750001-799999 | 1,700 | 10,470 | 4,850 | 2,250 | 8,800 |
| 800000-899999 | 1,500 | 11,970 | 4,850 | 2,250 | 8,600 |
| 900000-1000000 | 1,776 | 12,264 | 4,850 | 2,250 | 8,876 |
| 1000001-3000000 | 1,875 | 13,230 | 4,850 | 2,250 | 8,975 |
| 3000001-5000000 | 2,000 | 13,580 | 4,850 | 2,250 | 9,100 |
| **Deposit (TZS) (agents) Range** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| 0 - 20,000,000 | - | - | - | 100 | - |
| **MOBILE BANKING** | | | | | |
| **Withdrawal - Bank to Wallet (TZS)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | 500 | | | 1,200 |
| 100000.1-300000 | | 1,000 | | | 2,200 |
| 300000.1-500000 | | 2,000 | | | 3,200 |
| 500000.1-1000000 | | 3,000 | | | 4,200 |
| 1000000.1-3000000 | | 4,000 | | | 5,000 |
| 3000000.1-5000000 | | 4,500 | | | 7,500 |
| **Deposit (TZS) (Wallet to Bank)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 0 - 9,999,999,999 | - | FREE | | | - |
| **Air-time top-up** | - | FREE | | | - |
| **Utility payments** | - | FREE | | | - |
| **Balance inquiry** | - | 300 | | | 400 |
| **Mini-statement** | - | 300 | | | 500 |
| **Full account statement request** | - | 500 | | | 700 |
| **Cheque book request** | - | 600 | | | 700 |
| **AMBT internal transfers (same account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1 - 5,000,000 | - | - | FREE | | - |
| **AMBT internal outgoing transfers (other account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-750000 | | 500 | | | 750 |
| 750000.1-2000000 | | 500 | | | 1,000 |
| 2000000.1-5000000 | | 500 | | | 1,000 |
| **AMBT External outgoing transfers (Bank to Bank)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 100000.1-300000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 300000.1-500000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 500000.1-1000000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 1000000.1-3000000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 3000000.1-5000000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| **FOREIGN EXCHANGE TRANSACTION** | | | **TZS** | **USD** | |
| Telegraphic Transfer - Normal Customer (SWIFT) | | | N/A | Up to USD 55 | |
| TISS- Normal Customer | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| TISS-Staff | | | 6,000.00 | 2.10 | |
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | from 3.0% per month to 6.0% per month Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | | | from 3.0% per month to 5.0% per month- Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance method. | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | | | from 2.5% per month to 6.2% per month - Based on risk Profile/Risk Group of client - on reducing balance method | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | from 2.2% per month to 2.8% per month- Based on risk profile/Risk Group of client.- on reducing balance method | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20.40% | N/A | |
| **Loan Processing Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 3.70%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 2.90%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| **Application Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20,000.00 | N/A | |
| **Insurance Fee Annual** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 2.9% | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% | N/A | |





# RC atangaza msako wa makahaba

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

SERIKALI mkoani hapa, imetangaza msako dhidi ya wasichana wanaofanya biashara ya ngono.

Ni baada ya wazee kulalamikia kukithiri kwa biashara ya ngono mkoani hapa majira ya mchana na kusababisha kushuka kwa maadili kwa watoto kwa kuiga tabia hiyo mbaya.

Walitoa kilio chao juzi kwenye kikao cha wazee, machifu na viongozi wa dini kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Christina Mndeme kujadii maendeleo ya mkoa.

Walisema mmomonyoko wa maadili kwa vijana unazidi kuongezeka wakiwamo watoto wa kike kufanya biashara ya ngono, mchana kweupe huku wakitembea barabarani nusu utupu.

Waliiomba Serikali mkoani hapa kukomesha biashara hiyo ili kulinda maadili ya vijana.

"Biashara ya ngono hapa mkoani Shinyanga imekithiri sana, imekuwa ikifanyika hadi mchana kweupe, unakutana na mabinti wamevaa nusu utupu ni hatari sana kwa watoto na wajukuu zetu, ni vyema serikali ilione hili mapema na kulidhibiti," alisema Mzee Fuel Mrindoko.

Akijibu ombi hilo, mkuu huyo wa mkoa, alitangaza rasmi kuanza msako dhidi ya mabinti hao wanaojihusisha na biashara ya ngono na nyumba za wageni zinapokea wateja wa aina hiyo.

"Nawatangazia kiama wale wote wanaofanya biashara ya kuuza miili yao waache mara moja tuna anza operesheni ondoa Makahaba kila mitaa na kwenye nyumba za wageni," alisema Mndeme. Alisema watahakikisha wanafanya kazi hiyo usiku na mchana lengo likiwa kuhakikisha wanalinda maadili ya vijana ili kuepuka kuzalisha Taifa la watu wa hovyo.

Aliwaahidi wazee hao kuwa Serikali itaendelea kushirikiana nao kwa kila hatua ili kupata ushauri namna ya kuliongoza Taifa, kulinda maadili na kutatua changamoto zinazowakabili wazee ikiwamo kupata huduma za matibabu bure.



Kamanda wa Polisi mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi akionyesha kwa waandishi wa habari mjini Shinyanga juzi, bunduki aina ya Shortgun Pump Action yenye namba za usajili MV 95738 V iliyokuwa imeibiwa katika kijiji cha Mondo, wilayani Kishapu, pamoja na vitu vingine vya wizi vilivyokamatwa katika msako uliofanyika katika kipindi cha Disemba 21 mwaka jana hadi Januari 23 mwaka huu, ambapo watuhumiwa 76 wamekamatwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC afunga soko kwa kipindupindu

**Na Thomas Wandiba**, SAUT

MKUU wa Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Hassani Masala amefunga soko la mbogamboga katika Mwaloni Kirumba kutokana na kukithiri kwa uchafu na ugonjwa wa kipindupindu.

Kata ya Kirumba imetajwa kuongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa kipindupindu kutokana na uchafuzi wa mazingira sokoni hapo na baadhi ya chemba za vyoo za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUSA) kubomoka na kusambaza maji taka kwenye makazi ya watu.

Kufuatia hali hiyo, mkuu huyo wa wilaya alifika sokoni hapo juzi na kuwaamuru wafanyabiashara kuondoka na kuahidi kuwatafutia eneo lingine salama kwa ajili ya kufanyia biashara zao.

"Najua hapa mmekaa tangu mwaka 2008, lakini kwa mamlaka niliyopewa na Rais, napaswa kuwalinda wananchi kwa kutoa maagizo ya kuwapanga, hivyo niwaombe kuwa tutawatafutia eneo lingine lakini hapa tupishe kwa sababu hizo za kiafya nilizowaambia," alieleza Masala.

Masala alitoa fursa kwa wafanyabiashara hao kupendekeza eneo wanalotaka kwenda kufanya biashara kwa kile alichoeleza kuwa yuko tayari kuwasaidia ili waendelee kujipatia kipato.

"Tuelewane mimi siwafukuzi hapa tukubaliane, mpendekeze eneo mnalotaka kwenda ila mimi siwezi kuwapangia kwa hiyo tutakaa chini na viongozi wenu mwende mkafanyie biashara kama ni nje ya wilaya nitaongea na mkuu wa wilaya mnakokwenda awapokee bila masharti," alisisitiza Masala.

Akizungumzia kuhusu kipindupindu, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Dk.Samson Marwa, alisema hali katika vituo vya kupokea wagonjwa sio nzuri huku akitaja maeneo ikiwemo Kata ya Kirumba ambayo asilimia 50 ya wagonjwa waliolazwa kituo cha Afya Buswelu imetoka katika kata hiyo.

"Hadi sasa Kituo cha Buswelu tuna wagonjwa 39 tangu tulipompokea mgonjwa wa kwanza Januari, 9 mwaka huu, asilimia kubwa ya wagonjwa ni wanaume na asilimia 50 wanatoka katika kata hii ya Kirumba, hivyo tuhakikishe tunaendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu hatari," alisisitiza Dk. Marwa.

# Watakiwa kufungua mashauri mtandaoni kwa namba NIDA

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi wilayani Kahama mkoani Shinyanga imewataka wananchi wenye namba na Vitambulisho vya Taifa (NIDA) wenye mashauri kujitokeza na kuyasajili kwenye mfumo wa kuratibu mashauri (E-CMS) ili kurahisisha utendajikazi na ufuatiliaji wa mashauri yanayoendeshwa.

Wito huo umetolewa jana na Hakimu wa Mahakama hiyo, Edmundi Kente wakati wa Kilele cha Wiki ya Sheria yenye kauli mbiu isemayo 'Umuhimu wa dhana ya haki katika ustawi wa Taifa' inayoambatana na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu sekta zinazofanyakazi na mahakama.

Alisema mfumo huo umeanzishwa na Mahakama nchini ili kurahisisha utendaji kazi wake na kujua mwenendo wa mashauri yanavyoendeshwa.

Alisema kuwa mfumo huo unamtambua mwananchi mwenye namba na kitambulisho cha NIDA na unaweza kusajiliwa pia na mawakili waliosajiliwa kisheria.

Kente, alisema mfumo huo unasajili kesi zote kupitia kwa makarani wa mahakama, ofisi za mawakili waliosajiliwa kisheria kupitia mifumo yao ya E-Wakili na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, na unasaidia kutunza nyaraka zinazotolewa maamuzi na kupata taarifa muda wote wa kesi zinazoendelea na zilizopata ufumbuzi.

"Shauri lolote linalosajiliwa kwenye mfumo huu ninaliona na kumpangia hakimu, hivyo tunaondokana na kuendesha mashauri kwa kutumia makaratasi. Kutumia mfumo huu utarahisisha pia kukataa rufani kwa mteja anayehitaji," aliongeza Kente.

Alisema mwaka jana mashauri 705 yaliamuliwa na idadi hiyo

Mwenyekiti wa Mawakili Mkoa wa Shinyanga, Evodius Rwangobe, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuwakimbilia mawakili vishoka ambao hawajasajiliwa kwenye mfumo huo kwa kuwa wamekuwa wakichelewesha mashauri na wateja kukosa haki zao.



Ukurasa 12

**Wanawake walivyoingia mtaani na kugeuza taka za Dar fursa kuwa na maslahi ya kiuchumi**



Ukurasa 13

Jenerali Mkunda apewe maua yake sasa



Ukurasa 14

**Saudi Arabia yafungua duka la pombe baada miaka 70 marufuku**


# BUFE

IJUMAA JANUARI 26, 2024

Nipashe


# Awamu Sita na itikadi diplomasia uchumi, uwekezaji kwa ngazi zote

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais wa Cuba, Salvador Valdés Mesa, yuko nchini kwa ziara ya siku tatu na juzi akianza ziara, amekutana na mwenzake, Makamu wa Rais wa Tanzania, mchumi Dk. Philip Mpango.

Ni mwendelezo wa urafiki kindugu tangu zama zilizopita, kati ya Rais Fidel Castro na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

Ujio huo una unasaba wa moja kwa moja na suala na diplomasia uchumi, pia uwekezaji nchini, ikigusa sekta ya kilimo ambako nao Cuba wako juu duniani.

Hapo inagusa moja kwa moja uhusiano wa wasomi wa kuzalisha chakula, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na wenzao, Chuo Kikuu cha Artemisa nchini Cuba, huku sekta ya tiba na dawa nayo ikiangaliwa. Vilevile, wakati kuna ugeni nchini wa marafiki wa kisiasa na kimaendeleo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, yuko nchini Indonesia katika ziara yenye tafsiri ya diplomasia uchumi.

Kimsingi, vita vya kuwekeza ni vya wote kitaifa na suala la muungano lina nafasi yake kwa sura nyingi kisekta kama.

Elimu, Afya, na Kilimo cha kisasa kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi, kuchochea ukuaji uchumi endelevu na unaopunguza Umasikini.

Ni tafsiri kutoka kwa Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, pale alipomwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kufungua Mkutano wa Kimataifa wa Tathmini ya Muda wa Kati wa Mzunguko wa 20 wa Benki ya Dunia (IDA20 Mid-Term Review) unaohusisha wakopaji, nchi Wahisani na Menejimenti ya Benki ya Dunia, Zanzibar.



Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango akisalimiana na Makamu wa Rais wa Cuba, Salvador Mesa, baada ya kuwasili Ikulu Jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MTANDAO.**

Wakakutana kutathmini miradi inayotekelezwa katika nchi zenye kipato cha chini, kupitia fedha za mkopo na msaada zinazotolewa na Mfuko huo uliopo chini ya Benki ya Dunia.

Rais Dk. Mwinyi akasema, mfuko huo wa IDA umechangia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya Tanzania Bara na Zanzibar, ikiwamo ya nishati ya umeme vijijini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 200.

Pia, akataja kuwawezesha Watanzania milioni 2.5 kupata nishati ya umeme, pamoja na maboresho, pia ujenzi wa vituo vya afya na madarasa ya shule.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akasema kaulimbiu ya Mkutano huo wa IDA-20 ambayo ni 'Ukuaji Endelevu wa Uchumi, Kujenga Uthabiti na Kusaidia Maendeleo ya Mtaji wa Watu,' inalingana kikamilifu na vipaumbele vya Tanzania.

"Kujitolea kwa serikali yetu katika kuboresha miundombinu, kuwekeza katika rasilimali watu, na kukuza utawala bora, kumechangia kwa kiasi kikubwa mwelekeo wetu wa maendeleo.

"Pia, uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan umepiga hatua kubwa katika kukuza ushirikishwaji na kujenga uthabiti kupitia mipango mbalimbali ya maendeleo," anatamka Dk. Nchemba.

Ni mkutano uliowakutanisha zaidi ya wajumbe 300 kutoka nchi zinazonufaika na IDA, viongozi wa Benki ya Dunia, pamoja na Wafadhili wanaochangia Fedha katika Mfuko huo wa IDA, Rais wa Benki ya Dunia, Ajay Banga.

**KITUO CHA UWEKEZAJI**

Nchini, Kituo cha Uwekezaji (TIC) ndicho kimebeba dhana kitaifa ya utendaji kuhusu uwekezaji na tafsiri yake pana. Kwa kifupi ndio injini ya miradi na uwekezaji nchini.

Hadi sasa, TIC imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje kwa kushirikina na ofisi za kibalozi na ofisi za wakuu wa mikoa. Iko katika mfumo endelevu wa kupokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini.

TOC inaeleza, hiyo inatokana na serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ujenzi wa miundombinu wezeshi kama barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na umeme.

**INAENDELEA UK.14**

BIASHARA

# Wanawake walivyoingia mtaani na kugeuza taka za Dar fursa kuwapa maslahi ya kiuchumi

**Na Jenifer Gilla**

INAINGIA kwenye historia ya Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP) mwaka huu, COP28, dunia imeanzisha kampeni inayoitwa 'Waste to Zero Initiative', lengo ni suluhisho la kudhibiti taka zaidi kuzibadili kuwa fursa.

Mkakati uliopo, ni baada ya utafiti kubaini taka nyingi za majumbani na zinazotupwa holela, zinazalisha bidhaa nyingine ndogo na hewa aina ya 'methane.'

Utafiti uliochapishwa kwenye Mtandao wa Benki ya Dunia unafahamisha hewa hiyo ni hatari, ikichangia asilimia 16 ya hewajoto (GHGs), matarajio yaliyopo ni kwamba itaongezeka maradufu duniani, kufika tani bilioni 2.6 ifikapo mwaka 2050.

Umoja wa Mataifa unatamka kwamba, hadi sasa kinamama ndio waathirika wakuu kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni.

Ni ripoti inayotaja asilimia 70 kati ya watu bilioni 1.3 wanaoishi katika umasikini duniani. Kwa kifupi ni wastani wa watu milioni 910.

Vilevile asimilia 40 ya nyumba zenye umasikini kupindukia zinaongozwa na kinamamamama. Ni kundi hilo la kijinsia nalo linazalisha kwa wastani wa asilimia 50 hadi 80, lakini inapokuja katika suala la milki ya mali hizo, kinamama hao wanaambulia asilimia 10 pekee.



Kikundi cha Ushirika wa Wakusanya Taka Wanawake wa Kimara Bonyokwa wakiwa katika eneo la kazi. **PICHA: JENIFER GILLA**

### VIKUNDI VYAONGEA

Kwa kufahamu hatari itokanayo na hali hiyo, kinamama kikundi cha wanawake cha Ushirika wa Wakusanya Taka kilichopo Kimara, Dar es Salaam, kimeamua kuingia mitaani kukusanya taka na wanazitengeneza kuwa malighafi, hata kuzihamisha kuwa kipato.

Hadi sasa imetimu miaka miwili wanawaajibika kiuchumi, wakikusanya, kuhifadhi na kuchakata taka kwa mfumo wa kisasa, wanazigeuza mbolea na chakula cha mifugo; kuku na samaki.

Nipashe ilipofika katika ofisi za kikundi hicho, eneo la Bonyokwa, Dar es Salaam, ikashuhudia lundo kubwa la taka zimepangwa kwa makundi ya kuanza kuchakatwa, ziko mahsusi za kutupwa dampo kuu la Pugu, Dar es Salaam.

Mwenyekiti, Rehema Tamimu, anasema waliunda kikundi hicho mwaka mmoja uliopita, baada ya kupata mafunzo ya kuongeza thamani taka hizo kwa kutengeneza bidhaa nyingine ikitolewa na taasisi ijulikanayo kama Nipe Fagio.

> **"Kwa mwezi tunaweza kukusanya mpaka laki nane, japo haikidhi mahitaji yetu, ukijumlisha gharama za kupeleka taka Pugu na kurekebisha matoroli tunayotumia kukusanya mitaani.**

Anasema kabla ya kuanzishwa kikundi hicho, walikuwa wakikusanya taka na kuzitupa dampo bubu na mitaroni, kwa sasa wameshafahamu taka hizo kwao ni mali, hata ina nafasi kuwavusha kutoka daraja la umasikini walilo nalo.

Rehema anasema baada ya mafunzo, taasisi hiyo kwa kushirikiana na kituo cha serikali, Dar es Salaam City Centre, waliwafadhili kwa vitendeea kazi na kuwaunganisha na masoko, hali inayowapa nguvu za hatua zaidi kikazi.

"Tuliona uchafu ulikuwa umezagaa, watu wengi walikuwa wanatupa taka hovyo, zinatoa uchafu na harufu mbaya baada ya hapo tukapata ufadhili kwa wadhamini kutoka kwa taasisi ya Nipe Fagio, ambao kwa sasa wametuacha na hatuna mfadhilii mwingine.

### UZALISHAJI MALIGHAFI

Mjumbe wa kikundi hicho, Halima Muda, anaeleza kwamba wanapokusanya taka, wanazitenganisha katika makundi matatu; taka za plastiki wanaziuza kwa kampuni zinazotengeneza malighafi.

Taka za majumbani wanazitumia kutengeneza mbolea na wanaiuza kwa wakulima wa bustani, kwa bei ya Sh.10,000 kwa kilo. Pia, taka zitokanazo na matunda wanatengeneza wadudu aina ya maboti na kuwauzua wafugaji kuku na samaki, Sh.5,000 kwa kilo.

### SIRI YA FAIDA

Halima anasema kupitia shughuli hiyo, sasa wanapata faida mara mbili, kwani wakienda kuzikusanya kwenye nyumba wanalipwa Sh. 2,000 mpaka Sh. 5,000 kutegemea na hali ya kipato kwa mmiliki wa nyumba na taka zilizoko.

"Kwa mwezi tunaweza kukusanya mpaka laki nane, japo haikidhi mahitaji yetu, ukijumlisha gharama za kupeleka taka Pugu na kurekebisha matoroli tunayotumia kukusanya mitaani," anafafanua Rehema

Mwanakikundi huyo aneleza kuwa kazi hiyo imebadilisha maisha yake, kwa sababu ana ajira ya kudumu inayompatia Sh. 50,000 kwa wiki wakati zamani aliambulia Sh. 10,000 kutoka kwenye taka alizokuwa akikusanya kwenye nyumba za watu.

Anasema, pesa anazopata zinamsaidia kuwahudumia watoto wake chakula na mahitaji muhimu ya shule, akiba akihifadhhi benki, jambo ambalo halijawahi kuwapo maishani mwake zamani.

Mkusanya taka mwingine, Anusiata Mapunda, anasema ni kazi iliyomuwezesha kufungua biashara nyingine ya kufuga kuku wa nyama na mayai. Kabla hakuwa na uwezo huo. Anasema, pia pesa hiyo anaitumia kusomesha mtoto wake wa kiume katika shule ya serikali mkondo wa Kiingereza, ikiwa naye ni historia mpya ya kimaisha.

"Wakati nazoa taka tu, hela iliyokuwa ni ndogo, kwa siku haizidi Sh. 2000, lakini tangu niingie kwenye kikundi hicho kuanza kuuza chupa na kutengeneza mbolea, chakula cha samaki kwa wiki ninapata Sh. 50,000 hadi Sh. 60,000.

"Namudu kulipia mtoto wangu ada ya Sh.300,000 kwa mwaka kwa shule ya Kiingereza ya serikali," anasema.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bahati Mayoma, anaeleza ni ufafiti unaonyesha wazi kuwa asilimia 80 ya taka zinazokusanywa nchini ni plastiki.

Hapo ana ushauri: "Plastiki madhara yake yanafahamika na kwa sababu aina nyingi, zinawekwa na kurejeshwa, basi hili litumike kama fursa".

### CHANGAMOTO ZAO

Mdau Anustasia, anasema wanapokuwa wanakusanya taka kwenye nyumba za watu jamii inawaona kama watu wenye matatizo ya akili, wengine wakihisi kuwa ni wezi na kuwatolea maneno machafu.

"Tunapokuwa tumevaa yale mavazi machafu, halafu hatuna vifaa muhimu vya kututambulisha kama tupo kazini, jamii inatuona kuwa ni watu wa ajabu. Kuna siku nilitaka kuitiwa mwizi na watu wakihisi kuwa ni mwizi" anasimulia.

Msimamizi Mkuu wa kikundi hicho, John Yusuph anasema kuwapo kikundi katika Mtaa wa Bonyokwa, kumesaidia kuweka mazingira safi, mwanzo maeneo mengi yalizungukwa na taka za plastiki.

"Mji ulikuwa mchafu, kwenye mito ya maji kulikuwa kumejaa pampasi za kutosha, mwisho wa siku Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, akaja akatupa wazo na akatuletea mfadhili, akatupa elimu na akatujengea hicho kibanda unachokiona hapa," anasimulia.

Sasa rai yake ni kwamba, wadau na serikali wawaunge mkono kwa kuwapatia vitendea kazi vya kisasa kama, Mabuti, glovu na barakoa za kujikinga kazini, pia gari la kupeleka taka dampo kuu.

### TABIBU NA WADAU

Daktari Bingwa wa Tiba kutoka Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam, Willbroad Kyejo, anasema taka zinavyozagaa mitaani ovyo au kukusanywa kwenye dampo,zinasababisha maradhi ya milipuko kama kipindupindu na anayebeba jukumu la kuhudumia wagonjwa ni mwanamke.

"Wanawake hao wanafanya jambo la maana kukusanya taka, kwa sababu wanaiepusha jamii na magonjwa ya mlipuko, kwani zaidi ya asilimia 70 ya magonjwa yanatokana na uchafu," anasema

Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linaeleza kuwa Sheria ya Mazingira, imewapa mamlaka Halmashauri, wilaya na serikali za mitaa kusimamia ukusanyaji, uhifadhi na usafirishaji taka kwa lengo la kuziondosha kabisa kwenye jamii.

Ofisa Hifadhi wa Maliasili na Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Enock Tumbo, anasema takriban asilimia 96 ya tani 319,000 za taka za plastiki zinazozalishwa nchini Dar es Salaam kila mwaka hazisimamiwi.

Hivyo, anasema inahatarisaha usafi wa mazingira na usalama wa viumbe, Tumbo akifafanua hatua za serkali kwamba: "Inaimarisha ushirikiano na mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile HUDEFO, NIPE FAGIO na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufanya usafishaji, ukaguzi na mpango wa ufuatiliaji wa takataka baharini".

Anaendelea: "Halmashauri ya Jiji inafanya utafiti juu ya usimamizi wa taka ngumu na kuanzishwa kwa wakala, baina ya manispaa na wadau katika mkoa wa Dar es Salaam, pamoja na ujenzi wa vituo ukusanyaji taka na dampo la taka chini ya mradi wa DMDP, awamu ya pili unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na serikali..."

Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Human Dignity and Environment Care (Hudefo), Sarah Pima, ana ufafanuzi kwamba taka na hasa za plastiki zina hatari ya kudumu muda mrefu.

Sarah anashauri hatua za kuzijeresha kwa kuzalishwa kingine, akinena "kudhibiti hizi taka zinaweza kutumika kama fursa mbalimbali...kutengeneza urembo, mkaa na bidhaa nyingine kama mbolea iwapo tu uhifadhi wake utakuwa mzuri".

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Jenerali Mkunda apewe maua yake sasa






**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
(kulangwasos@gmail.com)

JANUARI 22 mwaka huu (2024) ni siku inayoweza kuandikwa na Watanzania kama moja ya siku za ufunuo kwao. Hiyo inatokana na kauli aliyoitoa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda.

Siku hiyo alikuwa akizungumza mbele ya Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais Samia Suluhu Hassan pale Lugalo, Dar es Salaam, kwenye Mkutano wa Mwaka 2023 wa Mkuu wa Majeshi na Makamanda.

Ni siku ya ufunuo, kwani Jenerali Mkunda alisema jambo ambalo pengine watu wangedhani lilikuwa la kumpelekea Amiri Jeshi Mkuu ofisini kwake

kimyakimya na kulifanyia kazi, lakini akaamua kuliweka hadharani akimulikwa na vyombo vya habari.

Endapo Mkuu wa Nchi asingekuwa anaamini katika falsafa ya uwazi na ukweli, jambo hilo lingemnyima raha na kumtesa akijisemea moyoni imemuadhiri, lakini ndiyo kwanza Rais akalipokea.

Katika kauli yake, Mkuu wa Majeshi aligusa moja kwa moja suala la wakimbizi na watafuta hifadhi walioko nchini miaka mingi na wanaoendelea kuingia, kwamba wamejichanganya na wazawa na kutoonekana kwa macho.

Mchanganyiko huo kwa mujibu wa Jenerali Mkunda, umefanya waajiriwe serikalini na hata wengine kuteuliwa katika nafasi mbalimbali za uamuzi.

Ieleweke kuwa nafasi za uamuzi ni za juu sana katika Taifa. Kwa tafsiri ya haraka ni kwamba yawezekana wapo ambao ni wabunge, naibu mawaziri, makatibu wakuu na hata mawaziri, waliongia nchini kama wakimbizi au watoto wa wakimbizi au watafuta hifadhi na kukita mizizi yao.

Jenerali Mkunda anapaswa kupewa maua yake, kwa kuja na hoja hiyo inayogusa moja kwa moja usalama na ulinzi wa nchi na hivyo kutufumbua macho, kwamba hatua zinapaswa kuchukuliwa sawia kuondokana na kadhia hiyo.

Ni jambo la kushukuru pia, kuwa Rais Samia pale pale alikiri kupokea hoja hiyo na kuahidi kuifanyia kazi kwa maslahi mapana ya taifa letu.

Tunajiuliza, hivi kama si Jenerali Mkunda kufunguka, nani angethubutu kumfunga paka kengele?

Kwa hali ya kawaida, wapinzani wangetakiwa kubeba hoja kama hii na kuipigia kelele, lakini wala! Hakuna aliyepata kujitokeza kulisemea ilhali linaonekana dhahiri.

Pengine nao wananufaika na ujio wa wakimbizi na watafuta hifadhi. Baada ya Rais kulipokea na kuahidi kulifanyia kazi, hapana sababu ya kulaumiana kuhusu nini kiini cha wakimbizi na watafuta hifadhi, tukijua fika kuwa historia ya nchi na viongozi waliokuwapo, ndiyo iliyotufikisha hapa.

Tanzania inajulikana tangu enzi hizo, kujali utu na haki za binadamu na hivyo kujiona haiko huru wakati Waafrika wengine na walimwengu kwa ujumla, wakiendelea kunyanyasika na ndiyo sababu ikajitolea kuwapokea.

Ukarimu huo ulishaigharimu kwa kupokea wahalifu, majangili na wauaji kutoka mataifa jirani, lakini pia uharibifu wa mazingira ukiwahusisha,

ingawa iliendelea kuwapokea, kuwalea huku waliokubali kurejea kwao wakifanya hivyo.

Ni jambo la aibu, kuona kuwa vijana wa nchi hii waliosoma na kuhitimu elimu ya juu, wakirejea mitaani kusaka kazi na kuambiwa wajiajiri, huku

baadhi ya ajira zikishikiliwa na waliokimbia kwao, kana kwamba walikotoka hakuna ajira.

Ni aibu zaidi, kuona wananchi wanaopigania Taifa lao, wakikosa nafasi za uongozi kwa sababu moja au nyingine na nafasi hizo kuishia kupewa wakimbizi na watafuta hifadhi katika nchi hii.

Jenerali Mkunda amefanya vizuri na kwa wakati mwafaka, ambao tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, ambao kuna wakimbizi wamekuwa wakichagua na kuchaguliwa bila wenyeji kutambua.

Inajulikana, baadhi yao wamekuwa wakigombea ubunge na hata kuteuliwa uwaziri, lakini waliowapigia kelele wakijua historia zao wakinyamazishwa na mambo kuendelea kama kawaida. Pengine ndiyo sababu ya kufunguka kwa Jenerali Mkunda.

Hivyo basi, kazi imebaki kwa Rais Samia, ya kuchekecha na kuengua pumba kwenye mchele, huku akikodolea macho zaidi Idara ya Uhamiaji, ambayo ndiyo hasa yenye jukumu la msingi la kuangalia nani anaingia nani anatoka.

Ikumbukwe idara hiyo ilishakubwa na utata wa namna hiyo huko nyuma! Tujiulize pia, inakuwaje wahamiaji haramu kila mara wanakamatwa kama

si Singida, Dodoma basi Iringa au Mtwara, wakiwa njiani kwenda Kusini mwa Bara la Afrika,

wengi wakitoka kama si Ethiopia ni Somalia, wanapita mipaka na njia gani mpaka kufika katikati ya nchi? Mama chekecha usichelewe, tukavuna mabua.

UCHUMI

# Saudi Arabia yafungua duka la pombe marufuku baada miaka 70

• Kigezo & masharti: Usindikizwe, kila mwezi una vipimo



Mteja wa vinywaji nchini Saudi Arabia. Hivi karibuni, nchi hiyo ilipandisha kodi ya vinywaji vyenye nishati, ili kupunguza kasi ya matumizi yake nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

**Riyadh, Saudi Arabia**

TAIFA la Saudi Arabia, limesema litafungua duka la pombe kwa wahamiaji maalum wasio Waislamu, mjini Riyadh, likiwa la kwanza kufunguliwa kwa zaidi ya miaka 70.

Wateja wa mgahawa huo watakuwa wafanyakazi wa balozi, ambao kwa miaka mingi wameagiza pombe kutoka nje katika vifurushi rasmi vilivyofungwa vinavyojulikana kama mifuko ya kidiplomasia.

Maofisa wa Saudia walisema duka hilo litakabiliana na wanachoendelea kukiita nchini humo, "biashara haramu ya pombe".

Marufuku ya kuuza pombe imekuwa sheria tangu 1952, baada ya mmoja wa watoto wa kiume wa Mfalme Abdulaziz, ambaye alikuwa amekunywa hadi kulewa kumuua kwa kumpiga risasi mwanadiplomasia wa Uingereza.

Duka hilo jipya litakuwa katika eneo linalopendwa sana na wanadiplomasia hao wa magharibi mwa katikati ya jiji, kulingana na waraka ulioonekana na mashirika ya habari ya kimataifa.

Chanzo kinachofahamu mipango hiyo, kimeviambia vyombo vya kigeni kwamba, duka hilo linatarajiwa kufunguliwa ndani ya wiki chache zijazo, hata hivyo kitaifa kazi kwa masharti.

Ili kuwa mdau wa duka hilo, mhusika anahitajika kujiandikisha kabla na kupokea kibali kutoka kwa serikali na ni marufuku kwa wadau wote wenye umri chini ya miaka 21, atakayeruhusiwa dukani na wakiwa katika mavazi yanayofaa na yanayoruhusiwa kwa staha.

Wanywaji husika hutakiwi kuandamana na msaidizi, kama vile dereva na kuna masharti ya kila mwezi

Hata hivyo, dai la waraka ulioonekana unadai masharti hayo hayatakuwa makali na watumiaji wataruhusiwa kunywa zaidi ya 'pointi' 240 za pombe kwa mwezi. Inataja lita moja ya vinywaji vikali, itakuwa na thamani ya pointi sita, lita moja ya divai pointi tatu na lita moja ya bia pointi moja.

Pia, hakuna mapendekezo kwamba wateja wataongezwa na kuorodhesha wageni "wa kawaida" Chini ya sheria ya sasa ya Saudi Arabia, adhabu za unywaji pombe zinaweza kujumuisha faini, kifungo cha jela, kuchapwa viboko hadharani na kufukuzwa nchini kwa wageni ambao hawajaidhinishwa.

Hati hiyo pia, inasema mamlaka inapanga mfumo mpya wa udhibiti ambao pia utaruhusu kiasi maalum cha pombe kuletwa na wanadiplomasia, ili kukomesha na kubadilisha mtindo usiodhibitiwa wa bidhaa kama hizo.

Kwa miaka mingi inatajwa wafanyakazi wa kidiplomasia wamelazimika kutumia "pochi" zao, ambazo haziwezi kuingiliwa na mamlaka katika nchi mwenyeji, kuleta kiasi kidogo cha pombe.

***• Kwa mujibu wa vyombo vya kimataifa.***

# Awamu Sita na itikadi diplomasia uchumi, uwekezaji kwa ngazi

**INATOKA UK.11**

Diplomasia ya uchumi nchini inapata uhamasishaji unaoifanya Tanzania kuwa kivutio katika kuwekeza barani Afrika na TIC ikifafanua imekuwa ikifanya uhamasishaji kimataifa.

Hapo inatoa mfano kati ya Juni 2021 hadi Julai 2022, kuna makongamano ya uwekezaji yaliyofanyika huko Doha, Qatar na ushiriki wake umeleta matokeo chanya, wawekezaji mbalimbali wakifika nchini.

Pia, nchini TIC inasema kuptoa tovuti yake, kwamba imekuwa ikiandaa miradi na kuinadi kwa wawekezaji, kupitia njia mbalimbali, vilevile iliandaa vikao na kampuni za wawekezaji watarajiwa nchini, wakipewa miongozo na taratibu za uwekezaji.

Kuna miradi kama ya kongani za viwanda katika sekta kama za kilimo, ikigusa mbolea, dawa, vifaa tiba, uvuvi na mifugo na kunadi wawekezaji wamejitokzea kuchukua fursa husika.

"Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuhamasisha diplomasia ya uchumi, itasaidia katika kuinua na kufanikisha uhamasishaji wa uwekezaji hapa nchini.

"Taswira nzuri inayofanywa kupitia ziara za Rais Samia Suluhu Hassan (za dilomasia uchumi) zinaleta sura kuwa Tanzania ni sehemu bora na inayofaa kuwekeza," inafafanua TIC kupitia taarifa za tovuti yake.

**VIKAO VYA DIASPORA**

Kituo cha Uwekezaji nchini kinatajwa kuandaa vikao vya diaspora nchini Misri na mataifa ya Scandinavia, kuwavutia wawekezaji wao. Pia, inasaidia wawekezaji wa ndani kuratibu uwasilishwaji wa miradi yao.

Pia, katika kipindi hicho kati ya Juni 2021 na Julai 2022 kuna ushiriki wake katika makongamano kama ya nchini: Kenya, Burundi, Ufaransa, Ubelgiji, Qatar, Uturuki, Afrika Kusini, na Algeria.

Vilevile, TIC inasema imeratibu na kushiriki makongamano ya biashara na uwekezaji kwa njia ya mtandao, kwa kushirikina na ofisi za kibalozi, taasisi za biashara na sekta binafsi nchini China, Japan, Nigeria, India, Qatar, Ujerumani, Canada, Pakistan, Italia, Algeria, Sweden na Vietnam

Kingine inataja kurahisisha mfumo wa utoaji cheti cha uwekezaji, huku kipindi cha kufanikisha huduma za usajili kurahisishwa kukamilisha mchakato wa usajili wa mradi, huku cheti cha uwekezaji kupatikana ndani ya siku tatu

**MWELEKEO WA UWEKEZAJI**

Katika kipindi kilichohitimishwa na bajeti ya mapato na matumizi ya serikali iliyoishia Juni 30 mwaka jana, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilijiwekea mwelekeo wa kuimarisha utoaji huduma zake sehemu moja au 'one stop facilitation centre'.

Hapo dira ikawa ni kuongeza usajili wa miradi, kuhamasisha uwekezaji na kuhudumia wawekezaji nchini katika kipindi tajwa.

Wakati hilo linafanyika, tayari kukaonekana kitaifa kuna mtiririko wa usajili wa miradi mipya inayowekekezwa ya sekta; viwanda, usafirishaji kilimo, ujenzi na majengo ya biashara, miundombinu ya kiuchumi, taasisi za fedha, rasilimali watu, usafirishaji, utalii na huduma.

Katika kufanikisha hayo, TIC ikaendelea kuboresha na kurahisisha utoaji huduma kwa wawekezaji nchini katika "One Stop kunakuwapo taasisi 12 za serikali zinazotoa huduma ikijumuisha Wizara ya Kazi, Wizara ya Ardhi, Uhamiaji, Mamlaka ya Kodi (TRA), Shirika la Viwango (TBS), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mamlaka ya Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), BRELA na TMDA.



# TIC yasaka wawekezaji wazawa nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KITUO cha uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili miradi 508 yenye thamani ya shilingi bilion 5.6 kwa mwaka jana inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini na kuwataka wananchi kuchangamkia ili kukuza Uchumi wao.

Meneja Uhamasishaji, Uwekezaji wa TIC, Felix John akitoa taarifa fupi ya majukumu yanayotekelezwa na kituo hicho, alisema uwekezaji huo unatarajia kuzalisha ajira 230,000 kwa vijana nchini.

John, alisema wamekuwa wakihamasisha watu kutoka maeneo mbalimbali kuhamasisha jamii kujitokeza kuwekeza na kuondoa dhana ya kuwa wawekezaji ni kutoka nje ya nchi pekee.

Aliitaja mikoa ambayo wamepita kuhamasisha uwekezaji kuwa ni ya kanda ya Kati, Ziwa, Kaskazini, Kusini na Mashariki ukiwamo Pwani na Morogoro. Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Benjamin Chikumba, alisema TIC inapaswa kupanua wigo wa wawekezaji ili kukuza uchumi na kuongeza ajira kwa vijana nchini.

Chikumba, alisema miradi iliyosajiliwa ni mingi, hivyo wanapaswa kuhamasisha wawekezaji wazawa kushiriki katika miradi kwa ajili ya utekelezaji.

Alisema serikali inaridhishwa na kazi hiyo inayofanywa na TIC, hivyo wanapaswa kuhimiza wawekezaji wazawa wajitokeze katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi TIC, Shami Mayosa, alisema fursa za uwekezaji zilizopo nchini zimeanishwa katika sekta za kilimo, ufugaji, utalii, uzalishaji ambazo zinagus kila eneo.

Mayosa, alisema TIC imejipanga kukuza uwekezaji kwa kuhamasisha uwekezaji wa ndani na uwezeshaji kupitia dirisha la pamoja.

Alisema wamekuwa wakitoa huduma za uwezeshaji katika nyanja za uwekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Prisca Dugilo, alisema wametenga maeneo makubwa kwa ajili ya uwekezaji mkoani mwake.

Prisca, amewahamasisha wawekezaji ndani na nje kuchangamkia fursa zilizopo Dodoma.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo akipanda mti kwenye eneo la shule ya msingi ya serikali ya mchepuo wa Kiingereza Dodoma, jijini Dodoma jana, kuashiria uzinduzi rasmi wa zoezi la upandaji miti kitaifa kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri Jafo aziagiza halmashauri kusimamia usafi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ,Dk. Selemani Jafo ameziagiza halmashauri nchini kusimamia usafi na utunzaji wa mazingira kwenye maeneo yao.

Dk. Jafo alitoa agizo hilo jana wakati akizindua zoezi la upandaji miti katika kuelekea Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliofanyika shule ya msingi ya mchepuo wa kiingereza ya Dodoma jijini hapa.

Aliyataja maeneo yanayopaswa kusimamiwa, kutunzwa na kufanyiwa usafi ni ya barabara, shule, taasisi na ya wazi ili kuongeza hewa safi.

Alizitaka wizara kuhakikisha zinaweka maofisa mazingira kwenye maeneo yao ili kusaidia kusimamia masuala ya mazingira kwenye wizara zao.

Alizihimiza kampuni na taasisi binafsi kupanda miti kwenye maeneo yanayowazunguka ili kuhakikisha yanavutia na kuwa na hewa safi.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma ,Jabir Shekimweri aliomba wadau wa mazingira nchini kuwasaidia vitendea kazi ili kufanikisha kazi ya utunzaji wa mazingira. Shekimweri alivitaja vifaa hivyo kuwa ni maboza ya maji kwa ajili ya umwagiliaji wa miti hasa katika kipindi cha kiangazi.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mkoa huo umejiwekea malengo la kupanda miti milioni 40 kwa kipingi cha miaka mitano ijayo kwa kila halmashauri ya wilaya miti milioni 1.5 kwa mwaka.

# 'Wananchi changamkieni fursa sekta ya mawasiliano'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKUU wa mikoa na wilaya wametakiwa kuhamasisha wananchi kuchangamkia fursa katika ujenzi wa miradi inayotekelezwa sekta ya mawasiliano nchini ili kuondokana na tatizo la ajira nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye kwenye uzinduzi wa kampeni ya utoaji elimu kwa umma kuhusu ujenzi wa minara 758 ya mawasiliano vijijini.

Nape alisema ufikishaji wa huduma ya mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini utachochea maendeleo.

"Hadi sasa Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imeingia mikataba na watoa huduma ya mawasiliano ili kufikisha huduma kwenye kata 1,974 zenye vijiji 5,111 nchini," alisema.

Alisema wananchi milioni 23 wanatarajiwa kufikiwa na huduma ya mawasiliano ya uhakika baada ya ujenzi wa minara hiyo kukamilika.

"Kujenga mnara ni gharama, mnara mmoja ni takribani shilingi milioni 350 na kuuendesha kwa mwezi kwa ile inayotumia mafuta ni shilingi milioni 1.8 na ile inayotumia umeme ni shilingi 400,000 bado hujalipa walinzi na mambo mengine," alisema Nape.

Alisema kutokana na uwekezaji wa serikali katika miundombinu ya mawasiliano unaofanywa kwa sasa, huduma hiyo itapatikana kwa gharama nafuu katika maeneo yote nchini. "Kutokana na hali hii, wito wangu kwa Watanzania kutumia mitandao hii kwa tahadhari kubwa ili isije kuwa sehemu baadhi yetu kufanya mambo yasiyo na maadili hali ambayo tutaijutia baadaye," alisema.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba alisema Mei 13, mwaka jana, Serikali kupitia mfuko huo uliingia mikataba ya kufikisha huduma za mawasiliano ya simu katika kata 713 nchini.

"Mradi huu wenye thamani ya shilingi bilioni 126, unalenga kufikisha huduma za mawasiliano ya simu (Sauti na intaneti/Data) katika kata 713 ambapo minara 758 itajengwa na kampuni mbalimbali za simu," alisema.

Alisema mpaka sasa minara tisa imejengwa katika mikoa ya Pwani, Tabora, Singida na Kigoma na kuanza kutoa huduma ya mawasiliano ya 2G, 3G na 4G.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi UCSAF, Profesa John Nkoma, alisema minara hiyo inajengwa vijiji kwa sababu ndiko asilimia kubwa ya wananchi wanaishi kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Nkoma, alisema baada ya ujenzi huo kukamilika, wananchi waishio katika maeneo hayo watanufaika na huduma ya mawasiliano.





# Ofisa ushirika abanwa kwa ubadhirifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC) imetoa wiki moja kwa Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe kutoa taarifa ya hatua alizochukua dhidi ya ubadhirifu kwenye vyama saba vya ushirika wilayani humo.

Agizo hilo lilitolewa na Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu TCDC, Isaiah Kapakala wakati akifungua mafunzo kwa viongozi wa vyama vya ushirika wa zao la tumbaku yanayofanyika katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya.

Kapakacha, alisema wamekuwa wakipata taarifa kwenye vyombo vya habari kuwa kuna malalamiko kwenye vyama vya ushirika vya wakulima wa ufuta kuhusiana na ubadhirifu na jinsi Mkuu wa Mkoa wa Songwe anavyotoa maagizo dhidi ya vitendo hivyo ambavyo vimekuwa vikiuchafua ushirika nchini.

"Hapa lazima tupate taarifa ya kinachoendelea ndani ya vyama hivi saba na hatua ambazo zimechukuliwa, mwezi huu hautakiwi kwisha maana kumekuwa na malalamiko mengi yakiwemo yanayohusu mbolea na hii inatuchafua," alisema Kapakala.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Songwe, Benjamin Mwangwala, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa viongozi wa vyama vya ushirika ili kuongeza ufanisi kwenye uendeshaji wa vyama hivyo.

Mwangwala, alisema mafunzo hayo yana lengo la kuwakumbusha viongozi hao majukumu yao na miiko ya uendeshaji wa taasisi zao.

# Uhamiaji waagizwa kushikilia pasipoti za makandarasi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

IDARA ya Uhamiaji Mkoa wa Mbeya imeagizwa kushikilia hati za kusafiria za makandarasi wa Kampuni ya MSAVM Bilgam ya nchini Uturuki hadi atakapokamilisha ujenzi wa mradi wa barabara kuu inayounganishwa na Bandari ya Ziwa Nyasa wilayani hapa.

Agizo hilo limetolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera wakati wa ziara ya kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo ya kukagua ujenzi wa mradi huo wa barabara hiyo ya Ibanda-Kanjunjumele- Itungi - Kiwira Port yenye urefu wa kilomita 32 na kubaini unasuasua.

Kabla Homera kuchukua uamuzi huo, Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Matari Masige alitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kuwa mpaka sasa.

Masige alisema kuwa mkandarasi ametumia zaidi ya asilimia 40 ya muda wa mkataba, lakini kazi haionekani tangu wakati huo, Homera alielezwa kuwa utekelezaji ulisainiwa Disemba 27, mwaka 2022 kati ya kampuni hiyo na TANROADS.

Alisema pamoja na kutumia muda huo, kazi iliyofanyika ni asilimia mbili pekee hali ambayo inaonyesha hana nia ya kukamilisha kwa wakati.

Alisema kwa mujibu wa mkataba wa mradi huo, mkandarasi anatakiwa kukabidhi kazi Machi 31, mwakani, lakini kutokana na kusuasua kwake, hawezi kukamilisha ujenzi huo.

Masige, alisema gharama za mradi huo ni Sh. Bilioni 38.5 na kwamba mkandarasi amelipwa Sh. bilioni tatu kama malipo ya awali kwa ajili ya kununua vifaa ambavyo hadi sasa hajanunua na badala yake anatumia magari ya kukodi. "Mheshimiwa mkuu wa mkoa tunaomba utusaidie maana mkandarasi huyu anakatisha tamaa, mpaka sasa amemaliza siku 298 kati ya siku 730 na mradi huu kwetu ni muhimu sana maana unatusaidia kuunganisha barabara kuu na bandari," alisema Matari.

Hata hivyo, alisema baada ya kubaini mkandarasi huyo anasuasua kufanya kazi, Wizara ya Ujenzi iliunda tume ambayo pia ilibaini hakuna kinachofanyika.

Baada ya maelezo hayo ya Meneja wa TANROADS, Homera alisema kuna uwezekano watendaji wa kampuni hiyo wakatoroka na kutekeleza mradi na ili kuwadhibiti wanatakiwa kupokonywa hati za kusafiria mpaka watakapokamilisha mradi.

Alisema hati zao zikishikiliwa hatua nyingine zinatakiwa ziendelee kuchukuliwa ikiwemo kupokonywa mradi na kumtafuta mkandarasi mwingine mwenye uwezo.

"Mimi sina mamlaka ya kukaa na hati za kusafiria za mtu yeyote, sasa naagiza Uhamiaji wilaya na mkoa mhifadhi hati za mkandarasi huyu, pia meneja wa TANROADS umwandikie barua Mtendaji Mkuu wenu na mimi nitamwandikia Waziri wa Ujenzi," alisema Homera.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema wakati mradi huo unaanza kuna wananchi walivunjiwa nyumba bila ya kulipwa fidia.

Kingamkono aliomba Serikali kufuata sheria kuvunja mkataba na mkandarasi huyo ili atafutwe mwenye uwezo wa kutekeleza mradi huo haraka ili wananchi waanze kunufaika.

Vilevile aliomba wananchi walioyunjiwa nyumba zao walipwe fidia ili waendelee na majukumu yao na ujenzi wa makazi mapya.



Mafundi ujenzi wakiendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mbeya inayojengwa wilayani Kyela, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Udumavu watoto chini ya miaka mitano tishio Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. Juma Mfanga amesema zaidi ya watoto 114,000 wenye umri chini ya miaka mitano mkoani hapa wamebainika kuwa na udumavu na kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao shuleni.

Dk. Juma Mfanga alitoa takwimu hizo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha lishe na mpango wa kupunguza udumavu mkoani hapa iliyofanyika Uwanja wa Polisi mjini Makambako.

Dk. Mfanga, alisema idadi hiyo ni sawa na asilimia 50.4 ya watoto hao ya wenye matatizo hayo.

Alisema asilimia 12 ya watoto hao wanakabiliwa na uzito pungufu na zaidi ya mbili ukondefu hali kutokana na lishe duni.

Kwa mujibu wa Dk. Mfanga, tatizo la udumavu kwa watoto linasababishwa na wazazi kushindwa kuwaandalia chakula bora na kuwalisha vya wanga ikiwemo makande na viazi huku muda mwingi wakitumia kwa shughuli za kiuchumi

"Na changamoto iliyopo pamoja na kwamba tuna makundi yote ya chakula kwenye mkoa, lakini hatuli chakula chenye mchanganyiko wa makundi sita ya hali hii inasababisha kuwepo kwa udumavu," alisema Dk. Mfanga.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Meckfrida Mmari, alisema changamoto kubwa ambayo inasababisha udumavu kwa watoto mkoani hapa ni wanaume kutelekeza familia na kusababisha wanawake kuhangaika na malezi.

"Wanaume tumetelekeza sana familia, unakuta huyo huyo mama ndiyo azalishe, baba akimbia kamuacha mama aangalie familia na familia haipati chakula bora au unakuta baba yupo lakini bado watu hawapati chakula bora," alisema Mmari.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji huo, Imani Fute, alisema kuna haja ya kutungwa sheria ya kuwabana wanaume kuhudhuria kliniki ili wapate elimu ya malezi kwa watoto toka wakiwa tumboni.

"Naamini waheshimiwa madiwani wenzangu tutaliwekea sheria suala la baba na mama kwenda kliniki tangu tunapoanza kugundua kuna mimba itakuwa ni lazima kwetu sote," alisema Fute.

Wakizungumza na Nipashe baada ya uzinduzi huo, baadhi ya wananchi walisema tatizo kubwa kwao ni namna ya kuandaa chakula bora na baadhi ya akina mama kuanza kuwalisha watoto wao uji na ugali katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo badala ya kuwanyonyesha.

Mkazi wa Makambako, Asifiwe Sanga, alisema kumpa mtoto vyakula mbadala zaidi ya maziwa ya mama kuna madhara mengi ikiwemo kupata vidonda vya tumbo.



# Jaji awafunda watendaji mahakama Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WATENDAJI wa mahakama visiwani hapa wametakiwa kufanya kazi kwa uadilifu na kuongeza nidhamu ili kuongeza imani kwa wananchi ya kupata huduma haraka katika idara hiyo.

Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla aliyasema hayo juzi wakati alipofanya ziara katika mahakama za Mkoa wa Kusini Unguja.

Jaji Khamis alisema nidhamu na uwajibikaji kwa watendaji wa mahakama unaweza kuharakisha kupatikana ufanisi kwenye taasisi hiyo hasa kuwahudumia wananchi.

Alisema mahakama ni taasisi inayotegemewa na wananchi kupata haki zao, hivyo bila ya watendaji kuwa na nidhamu na kuwajibika, watakuwa na shaka ya upatikanaji wa haki wanayoitafuta.

Jaji Khamis alitumia nafasi hiyo kuwaeleza watendaji na mahakama kuhakikisha wanajiepusha na vitendo vya rushwa ambavyo kwa kiasi kikibwa vinaivunjia hadhi taasisi hiyo.

"Mkiwa mnatuhumiwa kupokea rushwa wananchi hawatakuwa na imani na nyinyi na dhana itakayokuwepo haki inaweza kununuliwa. Kwa hiyo lazima mviepuke vitendo vya rushwa," alisisitiza.

Alisema ikiwa kila mfanyakazi atatoa ushirikiano na viongozi, hakutakuwa na migogoro ambayo itapelekea kushuka kwa nidhamu kazini.

Mrajis wa Mahakama Kuu, Valentina Andrew Katema, aliwataka mahakimu kuhakikisha mienendo ya kesi inapatikana kwa wakati ili wananchi wajenge imani na mahakama.

Alisema umefika wakati kesi hizo mara tu zinapowasilishwa mahakamani lazima kuwe na utaratibu wa kuandaa mashahidi ili zimalizike kwa wakati.

Wafanyakazi katika mahakama hizo walisema licha ya kufanyakazi kwa kujituma, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi na kushindwa kufikia malengo.

Ziara hiyo Jaji mkuu ni miongoni mwa utaratibu aliojiwekea kila mwaka kuzitembelea mahakama kusikiliza changamoto na kuzitatua.

Aidha katika ziara hiyo alikagua ujenzi wa jengo la Mahakama ya Mkoa wa Kusini liliopo Binguni.

# Vijana wanolewa kujiajiri, kuajiriwa

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Abdallah Hussein Kombo ameuagiza uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kushirikiana na wadau kupitia sheria za matumizi bora ya bahari ili kufikia vigezo vya kimataifa na kuongeza ajira kwa vijana visiwani hapa.

Kombo alitoa agizo hilo jana kwenye kikao cha mradi wa kuwajengea uwezo vijana kujiajiri na kuajiriwa katika Soko la Uchumi wa buluu Zanzibar kilichofanyika visiwani hapa.

Alisema sheria hizo hazikidhi haja kwa sababu sera ya matumizi ya bahari imebadilishwa na kwamba kuna haja ya sheria kuendana na matakwa ya matumizi ya bahari yanayotakiwa kwa sasa.

Kuhusu matumizi ya bahari, alihimiza kuwepo mtaala wa kuielimisha jamii namna bora ya kuitumia kwa ajili ya kuwawezesha watu wengi zaidi kufaidika na hazina hiyo.

Akizungumzia kuhusiana na uhifadhi wa mazingira, alisema kuna umuhimu wa kuweka kikosi cha kukagua usafi wa mazingira hasa ikizingatiwa kuwa zipo taasisi nyingi zinazohusika na ustawi wa matumizi bora ya bahari na rasilimali zake.

Makamu Mkuu wa SUZA, Profesa Mohammed Makame Haji, alisema chuo hicho kimepewa jukumu kuongeza nguvu katika ustawi wa uchumi wa buluu, kuvuna bidhaa za bahari na kudumisha uhusiano baina ya pande mbili.

Akiwasilisha mada katika kikao hicho, mratibu wa mradi huo kutoka SUZA, Dk. Yahya Hamad Sheikh, alisema mradi huo wa vijana kujiajiri na kuajiri katika Uchumi huio, utachangia kupunguza ongezeko la vijana wasiokuwa na ajira Zanzibar.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa vijana wasiokuwa na ajira visiwani hapa mwaka 2006 walikuwa 379,038 kutoka 568,094 mwaka 2021.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha idadi ya vijana hao wenye umri wa miaka 15 -35 imeongezeka kutoka asilimia 19.6 (2006) hadi asilimia 27.4 (2021).

Alisema wasichana wasiokuwa na ajira wanakadiriwa kufikia asilimia 40.6 kwa mwaka (2021) kutoka asilimia 15.4 (2006).

Raya Juma Khalfan, mwakilishi kutoka jumuia ya wanawake mabaharia alishauri kuwepo chuo cha mabaharia wanawake visiwani hapa ili kupunguza gharama za kwenda kusoma nje ya nchi.

Khamis Rashid ambaye ana uzoefu katika masuala ya ubaharia, alisema asilimia 80 ya mabaharia wa visiwani hapa wanatoka Tanzania Bara baada ya Zanzibar kuwaandaa vijana wengi mabaharia na kushindwa kuwatumia.

Mradi huu unaotarajiwa kugharimu shilingi bilioni 125, utagharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa asilimia 90 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) 10 umeanza utekelezaji Mei mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Septemba 2027.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba Zanzibar, Mwanaisha Ali Said akizungumza na wapangaji wa nyumba za Mombasa kwa Mchina, kuhusu ulipaji wa kodi kwa wakati katika kikao maalum kilichoandaliwa na shirika hilo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwarobaini rushwa ya ngono wapatikana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) itasaidia kutoa taarifa za rushwa ikiwemo ya ngono katika taasisi za serikali na zisizo za serikali na kutokomeza vitendo hivyo visiwani hapa, imefahamika.

Ni baada ya kuwapo kwa sheria madhubuti inayoipa uwezo kuchunguza makosa ya rushwa ikiwemo hiyo ya ngono kwa taasisi hizo na kutoa ulinzi wa kutosha kwa shahidi na anayetoa taarifa zaidi ya makosa hayo kutasaidia kuripoti makosa hayo katika chombo hicho.

Hayo yalisemwa jana na wanaharakati wa masuala ya wanawake na watoto katika kikao maalumu kati ya ZAECA, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, Zanzibar (TAMWA ZNZ).

Sheria ya kuzuia rushwa namba 5 ya mwaka 2023 kifungu cha 52 cha sheria hiyo, kinapinga rushwa ya ngono kwa ajili ya kupata huduma au kutotoa huduma na adhabu yake kifungo miaka saba jela au kisochozidi miaka 10 pamoja na faini isiyopungua Shilingi milioni 20.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi Idara ya Kinga wa ZAECA, Bakar Hassan, alisema wamejipanga kutoa elimu ili sheria hiyo iweze kujulikana na wananchi.

Alisema wananchi wanapaswa kuelimishwa kuwa ZAECA ina mamlaka kushughulikia kesi hizo kwa usiri na kutoa adhabu hadi kwa maofisa wanaokiuka maadili ya kazi yao.

Hassan alinukuu kifungu cha 52-(1) kuwa mtu ambaye atashawishi, kukubali au kuahidi kutoa rushwa kwa ajili ya kupata huduma atakuwa ametenda kosa.

Alisema ni muhimu wananchi kujiepusha kutenda makosa hayo kwani yanawanyima haki hasa wa hali ya chini kupata ajira, vyeo na haki nyingine.

Mkurugenzi wa TAMWA ZNZ, Dk Mzuri Issa alisema wanawake na wasichana wanakabiliwa na changamoto kubwa kufikia ndoto zao za maendeleo kutokana na rushwa ya ngono kwa kukosa mahali pa kukimbilia.

Dk. Mzuri alisema kuanzishwa kwa sheria mpya ya ZAECA kutafungua ukurasa mpya katika mapambano ya rushwa hasa ya ngono katika nafasi za kazi za kitaifa na za kisiasa na hasa kuelekea katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Mkurugenzi wa ZAFELA, Jamila Mahmoud, alisema ni vyema elimu ya rushwa ya ngono ikatolewa tokea ngazi ya chini ikiwemo kwa wanafunzi shuleni ili kufahamu madhara yake.

Alisema ni vema ZAECA ikajipanga zaidi ili wananchi waongeze imani yao kwao baada ya kupata mahali pa kukimbilia wakifikwa na kadhia hiyo kuepuka kudhalilishwa.

TANGAZO

BancABC part of atlasmara

# AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31 Dec 23 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30 Sep 23 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,876 | 5,466 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,369 | 12,626 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 42,324 | 45,516 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,125 | 18,097 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 171 | 350 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 87,183 | 92,216 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 131,562 | 130,210 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 15,004 | 16,622 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,630 | 2,020 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **303,244** | **324,123** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 25,212 | 34,365 |
| 18 | Amana za Wateja | 147,688 | 159,968 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,005 | 3,370 |
| 28 | Madeni | 102,154 | 100,789 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **279,059** | **298,491** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **24,185** | **25,632** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 139,306 | 139,306 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 322 | 409 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (114,749) | (114,835) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,551) | (2,266) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 2,856 | 3,018 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **24,185** | **25,632** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 7,503 | 5,911 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,110 | 7,492 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,111 | 4,242 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 7.98% | 7.91% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.50% | 5.57% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 78.47% | 69.19% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 43.39% | 40.17% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 45.59% | 48.70% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -11.03% | 5.76% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -6.44% | 4.43% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31 Dec 23 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 31 Dec 22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 Dec 23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 Dec 22 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,974 | 10,571 | 42,483 | 40,899 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,659) | (5,115) | (18,969) | (19,878) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6,315** | **5,457** | **23,514** | **21,020** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 234 | (1,494) | 1,287 | (4,943) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (750) | (1,340) | (2,006) | (1,150) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **972** | **3,045** | **5,672** | **9,021** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 235 | 253 | 1,783 | 905 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 429 | 324 | 1,335 | 8,116 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 309 | 2,468 | 2,554 | - |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,998)** | **(8,006)** | **(31,783)** | **(30,681)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,921) | (3,065) | (11,400) | (10,991) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | (1,642) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,076) | (4,941) | (20,383) | (18,048) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,226)** | **(2,338)** | **(3,316)** | **(6,733)** |
| **9** | Tengo la Kodi ya Mapato | (59) | (65) | (235) | (10,537) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,285)** | **(2,403)** | **(3,551)** | **(17,270)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,285)** | **(2,403)** | **(3,551)** | **(17,270)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 171 | 177 | 171 | 177 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.52) | (0.98) | (0.36) | (2) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.64% | -2.94% | -1.13% | -2.12% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -20.64% | -38.02% | -14.26% | -58.39% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 109.75% | 94.16% | 108.90% | -102.13% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.38% | 3.06% | 3.14% | 1.86% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Dec 23 | Robo Mwaka iliyopita 30 Sep 23 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,226) | (490) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,586 | 1,650 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,353) | (1,589) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (21,432) | 10,587 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 3,192 | (9,729) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 635 | (840) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 886 | (774) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (59) | (59) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(17,771)** | **(1,243)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,446) | (50) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,446)** | **(50)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 1,365 | 4,539 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **1,365** | **4,539** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (17,852) | 3,246 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 128,405 | 125,159 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **110,553** | **128,405** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | - | **(114,427)** | - | - | **3,018** | **11,746** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (3,551) | - | - | - | **(3,551)** |
| Hisa za upendeleo | 16,352 | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (322) | 322 | - | (162) | **(162)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **139,306** | - | **(118,299)** | **322** | - | **2,856** | **24,185** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | - | **(99,102)** | **2,162.58** | - | **989** | **27,004** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (17,288) | - | - | - | **(17,288)** |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 2,029 | **2,029** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 2,163 | (2,163) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | - | **(114,427)** | - | - | **3,018** | **11,746** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 26 Jan 24 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 26 Jan 24 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 26 Jan 24 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 26 Jan 24 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 26 Jan 24 |

## HABARI KIMATAIFA

# ICJ kutoa hukumu kesi dhidi ya Israel

**The Hague,** Uholanzi



MAHAKAMA ya kimataifa ya haki (ICJ) inatarajiwa leo kutoa hukumu katika kesi ya mauaji ya kimbari iliyofunguliwa na Afrika ya Kusini dhidi ya nchi ya Israel.

Hukumu hiyo ambayo inasubiriwa kwa hamu duniani kote, itatolewa na mahakama hiyo ambayo ni chombo cha kisheria cha Umoja wa Mataifa baada ya Afrika Kusini kudai katika mashtaka hayo kuwa mashambulizi yanayofanywa na Israel katika eneo la Ukanda wa Gaza ni sawa na mauaji kimbari dhidi wa Wapalestina.

Mahakama hiyo yenye makazi yake katika mji wa The Hague, nchini Uholanzi inaweza kuagiza Israeli kusitisha mashambulizi yake ya kijeshi katika eneo hilo,.

Mapigano hayo yalianza Oktoba 7, mwaka jana baada ya wanamgambo wa Hamas kufanikiwa kuingia ndani ya Israel na kuwauawa watu zaidi ya 1000 na wengine 240 kuchukuliwa mateka.

Katika kesi hiyo, majaji 15 wanasikiliza na kuchunguza madai hayo yanayoelekezwa dhidi ya Israel.

Katika madai ya Afrika Kusini inataka ICJ kuilazimisha Israel kusitisha operesheni zake za kijeshi ndani ya Gaza, na ilisema nchi hiyo inafanya mauaji ya kimbari dhidi ya Wapalestina.

Aidha imeiambia mahakama hiyo iyazingatie matendo hayo ya Israel kwenye ardhi hiyo ya Wapalestina yanaendana na mkataba wa Kimataifa wa kuzuia mauaji ya kimbari uliopitishwa mwaka 1948.

Kulingana na mkataba huo, mauaji ya kimbari ni matendo yanayosababisha vifo vya watu wengi kwa lengo la kusambaratisha kwa sehemu au kwa jumla, taifa zima, kabila au jamii ya watu wa rangi ama dini moja.

Afrika Kusini na Israel zote zimesaini mkataba huo ambao unazilazimisha kutofanya mauaji ya kimbari na pia kuyazuia na kuyaadhibu.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kusikilizwa kwa kesi hiyo mwezi uliopita, wakili wa Mahakama Kuu ya Afrika Kusini, Adela Hassim, alisema shambulizi la Oktoba 7 la Hamas, haliwezi kuhalalisha Israel kuvunja Mkataba wa mauaji ya Kimbari.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisema hatua yao ya kupinga mauaji ya watu wa Gaza, iliwasukuma wao kama nchi kufungua kesi ICJ.

Wakati huo huo, mji wa Khan Younes, ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza, umeendelea kutikiswa na mabomu yanayoangushwa na ndege za Israel.

Mji huo ambao sasa umekuwa kitovu cha mapigano kati ya jeshi la Israel na Hamas.

Juzi jengo la Umoja wa Mataifa ambalo lilikuwa likitumika kuwahifadhi watu waliokimbia makazi yao lilishambuliwa na kusababisha vifo vya watu kadhaa.

Hata hivyo, nchi za Qatar, Misri na Marekani zinajaribu kupatanisha pande hizo zinazopigana ili kufikia mapatano mapya ambayo yatakuwa na muda mrefu.

Lakini kituo cha habari cha Israel cha 12, kilimnukuu Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, alisema hana imani na nchi ya Qatar kuwa mpatanishi. **RFI**

# Sita wahukumiwa kifo Ghana kutaka kuipindua serikali

**ACCRA,** Ghana

RAIA sita wa Ghana wakiwemo wanajeshi watatu wamehukumiwa kunyongwa hadi kifo baada ya kupatikana na hatia ya kula njama ya kupindua serikali miaka mitatu iliyopita.

Kesi hiyo ni ya kwanza ya uhaini kuendeshwa nchini Ghana tangu 1966 wakati kiongozi aliyepigania uhuru Kwame Nkrumah alipopinduliwa.

Watu hao sita walikamatwa 2021 katika mji mkuu wa Accra wakati walipokuwa wakifanya silaha ambazo zingetumika katika mapinduzi hayo.

Awali washtakiwa hao, akiwemo mfua bunduki, walikana kuhusika na tukio hilo.

Mawakili wa utetezi waliiambia mahakama kuwa watakata rufaa dhidi ya uamuzi huo katika Mahakama ya juu.

Watu wengine watatu, akiwemo ofisa mkuu wa polisi na askari wawili wa kijeshi, waliachiliwa huru.

Kulikuwa na ulinzi mkali nje ya Mahakama Kuu mjini Accra wakati wa kutolewa kwa hukumu siku ya Jumatano.

Kulinagana na stakabadhi za Mahakama inaeleza watu hao walikamatwa wakiwa na bunduki zinazotengenezwa kienyeji, vilipuzi vya kujitengenezea na bunduki aina ya AK-47.

Waendesha mashtaka wa serikali walisema kundi hilo lilikuwa na mpango wa kuandaa maandamano ambayo yangesababisha serikali kupinduliwa n serikali ya Rais Nana Akufo-Addo kabla ya uchaguzi mkuu wa 2020. **BBC**

## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

# Malale afurahia ushindani JKT TZ

Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Malale Hamsini, amesema anafurahishwa na ushindani uliopo wa kuwania namba katika kikosi chake ambao anaamini utasaidia kupata matokeo chanya kwenye mechi za Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kuendelea hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe jana, Malale alisema kila mchezaji anapambana kuhakikisha anapata namba na hali hiyo inapelekea kupandisha viwango vyao.

"Ushindani uliopo ndani ya timu yangu unanipa faraja ya kutarajia mabadiliko makubwa kwenye michezo yetu ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayoanza mwezi ujao," alisema Malale.

Kocha huyo aliongeza ligi hiyo ina ushindani mkubwa na ili kujiandaa na duru la lala salama analazimika kucheza michezo minne ya kirafiki ili kujiimarisha.

"Nimeanza mazungumzo na baadhi ya timu za Ligi Kuu pamoja na Ligi Daraja la Kwanza (Ligi ya Championship), ambazo ninaamini kiufundi nikijipima nazo zitanisaidia kuimarisha wachezaji wangu," Malale alisema.

Aliongeza wachezaji wote wanaendelea vyema na mazoezi habari njema nyota waliokuwa majeruhi akiwamo kiungo, Hassan Dilunga, wameanza kufanya mazoezi mepesi.

"Dilunga ameanza kufanya mazoezi mepesi mepesi baada ya mwezi mmoja atakuwa amekaa sawa kwa ajili ya kuungana na wachezaji wenzake ili kuipigania timu, tunasubiri kupata mchango wake," aliongeza kocha huyo.

# MWAKINYO AAHIDI FURAHA ULINGONI ZANZIBAR KESHO

Na Shufaa Lyimo

BONDIA Hassan Mwakinyo amewatoa hofu mashabiki wa ngumi nchini na kusema amejiandaa vyema kuonyesha kiwango cha juu katika pambano lake dhidi ya Mbiya Kanku kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

**Mwakinyo pia amethibitisha pambano hilo litachezwa kama lilivyopangwa na kuwataka wadau kupuuza tetesi za kutofanyika kwa mchezo huo.**

Pambano hilo la kimataifa lililopewa jina la 'Mtata Mtatuzi' ambalo ni maalumu katika sherehe za kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar litafanyika kesho kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, ulioko Zanzibar.

Maandalizi kuelekea pambano hilo la raundi 10 kuwania mkanda wa Dunia WBO yamekamilika.

Akizungumza jijini, Dar es Salaam jana, Mwakinyo, alisema amejipanga kuonyesha uwezo wake wa juu kwa sababu anahitaji kupata ushindi na kuwapa burudani mashabiki wa ngumi.

Mwakinyo alisema amejipanga kuonesha mchezo ambao wengi hawajahi kuuona huku , akiahidi kutoa burudani kwa mashabiki wake.

"Kuna baadhi ya watu wanamtumia ujumbe mpinzani wangu asikubali kupambana ili pambano liharibike, ionekane ni kawaida yangu kuharibu pambano, jambo ambalo si kweli, tumeshakubaliana na promota na kama itatokea hivyo, nitapigana na promota mwenyewe ilimradi watu wapate burudani," alisema Mwakinyo.

Aliongeza amefanya mazoezi kwa muda mrefu hivyo ana hamu ya kuonyesha mashabiki wa mchezo huo makali yake na anaamini wengi watafurahia pambano hilo.

Mabondia wengine watakaopanda ulingoni katika mapambano ya utangulizi watakuwa ni kati ya Hemed Pelembela dhidi ya Fikiri Mohammed, Hussein Itaba atadundana na Juma Misumari huku Bakari Bakari ataonyeshana ubavu na Seleman Hamad wakati Masoud Khatibu atapambana na Yahaya Khamis.

Kwa upande wa wanawake, Debora Mwenda kutoka jijini, Mbeya atapambana na Zulfa Yusuph wa Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Bunge Bonanza, Festo Sanga pamoja na wawakilishi wa Yanga na Simba, Mkurugenzi wa Hazina wa Benki ya Azania, Gilbert Mwandimila (wa pili kulia) wakionyesha vifaa vitakavyotumika katika bonanza hilo litakalowahusisha wabunge na wafanyakazi wa Bunge ambao ni mashabiki wa klabu hizo kongwe litakalofanyika kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# *New City yatarajia makubwa Ligi Kuu Bara*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya New City FC imesema inatarajia kufanya vizuri katika mechi zake za mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu Zanzibar ili kufidia makosa waliyoyafanya mapema msimu huu, imeelezwa.

New City FC ni moja ya timu ambazo hazikufanya vyema, ikipoteza mechi saba kati ya michezo 15 waliyocheza katika mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Razak Rajab, alisema kikosi chake kimesajili wachezaji wenye uwezo ambao wataziba mapengo waliyoyaona katika mzunguko wa kwanza.

Razak alisema wamenasa wachezaji wapya saba ambao wana uzoefu na wanaifahamu vyema ligi hiyo, hivyo wanaamini watasaidia timu kufikia malengo.

"Tumeboresha maeneo ambayo yalikuwa na changamoto kubwa katika timu yetu iliyopelekea kutopata matokeo mazuri, hasa eneo la mlinda mlango, mastraika, viungo pamoja na walinzi, tumesajili wachezaji ambao wataenda kufanya kazi tunayoitarajia hatimaye tutajilinda na janga la kushuka daraja," alisema Razak.

Aliongeza kupitia michezo ya kirafiki ambayo wamecheza, amepata nafasi ya kuona uelekeo wa kikosi chake ambacho tayari kimeanza kupata muunganiko kati ya wachezaji wapya waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo na wale wa zamani.

"Nimefurahishwa na hali ya ushindani wa wachezaji wangu, wale wapya wameanza kuzoeana na wenzao, hii ni dalili njema katika kikosi chetu, tunahitaji kupata matokeo chanya na kurejea kwenye malengo yetu," Razak alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 16, New City FC yenye pointi 16 iko kwenye nafasi ya 12.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati bingwa wa michuano ya Kombe la ZFF huenda kupeperusha bendera ya visiwa hivyo katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Timu nne zitakazomaliza katika nafasi ya chini katika ligi hiyo zitashuka daraja na kuelekea Ligi Daraja la Kwanza kwa kanda walizitoka (Unguja na Pemba).

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KIMMICH ANUKIA ENGLAND

LIVERPOOL wameungana na Manchester City katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joshua Kimmich, 28, kutoka Bayern Munich. ***(Bild)***

### UNITED KUMSUBIRI MARTIAL

KLABU ya Manchester United haitaraji kusajili mbadala wa fowadi wa Ufaransa, Anthony Martial, 28, ambaye anatarajiwa kuwa nje kwa wiki 10 baada ya kufanyiwa upasuaji wa paja. ***(Mail)***

### MAN U KUREJESHA MKWANJA

MANCHESTER United wanapanga kurejesha pauni milioni 100 katika mauzo ya wachezaji msimu huu wa joto, wakianza na mshambuliaji, Mason Greenwood, 22, ambaye yuko kwa mkopo Getafe. ***(i Sports)***

### VALDIMARSSON SOKONI

KLABU ya Brentford imekubali ada ya pauni milioni 2.6 kutoka Elfsborg ya Sweden ili kumnasa mlinda mlango wa Iceland, Hakon Valdimarsson, 22. ***(Subscription Required)***

### GODFREY KUTUA GENOA

KLABU ya Serie A, Genoa inavutiwa na beki wa Everton, Ben Godfrey, 26. ***(Fabrizio Romano)***

### ONANA AKARIBIA NEWCASTLE

EVERTON pia wako tayari kumuuza kiungo wa kati, Amadou Onana, 22, mwezi huu kwa Newcastle United inayomwania kwa ada ya pauni milioni 60. ***(Football Transfers)***

### LUTON YAMTAKA SHEAF

KLABU ya Luton Town inavutiwa na kiungo wa kati wa Coventry City, Ben Sheaf, 25. ***(Team Talks)***

### CORDOBA HAKIJAELEWEKA

KLABU ya Fulham imejiondoa kwenye mazungumzo na Krasnodar kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Cordoba, 30. ***(Mail)***

### TRIPPIER ATUA BAYERN

BAYERN Munich wamemaliza harakati zao za kumsajili beki wa kulia wa Newcastle United na England, Kieran Trippier, 33. ***(ESPN)***

### SIMONS ATAJWA ARSENAL

ARSENAL wanasaka dili la kumnunua kiungo mshambuliaji wa Paris-St Germain, Xavi Simons, 20, ambaye yuko kwa mkopo na RB Leipzig, kama mbadala wa kumnunua fowadi wa Wolves Mreno Pedro Neto (23). ***(Football Transfers)***

### DUBRAVKA NJIA PANDA

GOLIKIPA wa Newcastle United kutoka Slovakia, Martin Dubravka, 35, anafikiria mustakabali wake katika klabu hiyo msimu huu wa joto. ***(i Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MO SALAH RASMI AREJEA LIVERPOOL

**Nahodha huyo wa Misri afuata matibabu England na...**

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah amerejea England salama kupata matibabu kutokana na jeraha lake la misuli ya paja, Shirikisho la Soka la Misri (EFA), lilithibitisha jana, ingawa haijulikani ni lini tena atajiunga na Timu ya Taifa kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), inayoendelea nchini Ivory Coast.

**Nyota huyo wa Liverpool alichechemea mwishoni mwa kipindi cha kwanza cha sare ya mabao 2-2 kati ya Misri dhidi ya Ghana, mechi iliyochezwa Januari 18, mwaka huu, na hapo awali aligundulika kuumia msuli wa paja ambao ulitarajiwa kumweka nje katika mechi mbili zilizofuata za Mafarao hao.**

Baadaye ilipendekezwa jeraha lake lilikuwa kubwa zaidi kuliko ilivyotarajiwa, na hatimaye ikaamuliwa Salah atahudumiwa vyema kwa kurejea Liverpool ili kufanyiwa matibabu makubwa zaidi.

Misri wamethibitisha kwa ESPN, Salah aliwasili England mapema Jumanne, lakini walikiri hawakuwa na uhakika kuhusu ni lini ataweza kurejea Ivory Coast.

"Salah alisafiri jana (juzi)," Ofisa Habari wa EFA, Mohamed Murad, aliiambia ESPN hapo juzi na kuongeza; "Hatujui tunaweza kumtarajia kurudi lini.

"Salah ni mchezaji mzuri, na mchezaji ambaye kila mtu nchini Misri anampenda," aliongeza. "Tulimtarajia kuwa hapa pamoja nasi."

Shirikisho la Misri lilitabiri hapo awali Salah anaweza kurejea uwanjani punde tu hatua ya robo fainali ya AFCON iliyopangwa kuchezwa kati ya Februari 2 na 3, iwapo mabingwa hao mara saba watatinga hatua ya nane bora.

"X-ray ambayo nahodha huyo wa Misri alifanyiwa ilionyesha Salah alipata mkazo kwenye misuli ya nyuma, na atakosa mechi mbili zijazo za timu hiyo kwenye AFCON dhidi ya Cape Verde, na kisha mechi ya hatua ya 16 bora," ilisomeka taarifa ya awali iliyotolewa na shirikisho hilo.

Baadaye, mwakilishi wa mchezaji huyo, Ramy Abbas Issa, alitoa mtazamo usio na matumaini juu ya jeraha la mshambuliaji huyo.

"Jeraha la Mohamed ni mbaya zaidi kuliko ilivyofikiriwa awali na atakuwa nje kwa siku 21 hadi 28, na sio michezo miwili," Issa alichapisha kwenye mtandao wa X Jumatatu iliyopita.

"Nafasi yake nzuri zaidi ya kushiriki AFCON ya sasa ni kufanyiwa matibabu makubwa nchini England na kujiunga na timu mara tu atakapokuwa fiti."

# KIVUMBI 16 BORA AFCON

**ABIDJAN,** Ivory Coast

HATUA ya mtoano wa timu 16 bora katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), itaanza kesho baada ya kukamilika kwa michezo ya hatua ya makundi juzi usiku.

Hatua ya makundi ilitoa kila kitu kutokana na matokeo ya mshtuko, mabao, rekodi, historia na mashabiki wenye shauku kujitokeza kwenye viwanja vya mechi.

Katika hatua hiyo ya mtoano wa 16 bora, mabingwa watetezi, Senegal watamenyana dhidi ya wenyeji wa mashindano hayo, Ivory Coast.

Tembo hao walipata kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Equatorial Guinea katika mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi, lakini bado walisonga mbele kama moja ya timu zilizomaliza nafasi ya tatu bora kwenye kundi.

Sasa wanakabiliwa na kibarua kigumu cha kuishinda Senegal ambayo haijapoteza mchezo wowote hadi sasa.

Vigogo wengine wawili wa Afrika watagongana wakati Nigeria itakapokutana na Cameroon, timu zote mbili zilikuwa na hatua za makundi zisizo za kuvutia, lakini zimebakia kuwa vinara.

Kwingineko, Morocco waliongoza kundi lao bila kufungwa watajaribu kuendeleza hali yao nzuri dhidi ya Afrika Kusini.

Baada ya kushinda kwa mshangao Kundi A bila kushindwa, Equatorial Guinea itajaribu kusababisha tafrani nyingine dhidi ya Guinea.

Washindi wa kwanza wa mtoano Namibia wanakabiliwa na changamoto kali kutoka kwa Angola.

Licha ya matokeo duni ya hatua ya makundi, Misri kama taifa lenye mafanikio zaidi kwenye micnuano hiyo itacheza na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mchuano mwingine wa kuvutia utashuhudia Mali ikimenyana na Burkina Faso huku Cape Verde itavaana na Mauritania.

## *Algeria, Tunisia, Ivory Coast yatimua makocha*

**KARHOGO,** Ivory Coast

ALGERIA imeachana na Kocha, Djamel Belmadi na Jalel Kadri, amejiuzulu kama Kocha wa Tunisia baada ya nchi zote mbili kutolewa katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), katika hatua ya makundi.

Kujiondoa kwa Belmadi kulikuja siku moja baada ya Mbweha hao wa Jangwani kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Mauritania, jambo ambalo lilimaanisha washindi wa 2019 walimaliza mkiani katika Kundi D.

Kadri alitangaza kujiuzulu katika mahojiano ya televisheni baada ya mechi ya Tunisia kutoka suluhu na Afrika Kusini katika mchezo wao wa mwisho wa Kundi E mjini Korhogo hapo juzi.

"Ujumbe wangu mkuu wa timu ya taifa ya Tunisia sasa umekwisha," Kadri anaripotiwa akisema.

Belmadi alichukua nafasi ya ukocha wa Algeria Agosti, mwaka 2018 na kutia saini nyongeza ya mkataba mwaka mmoja uliopita ili abakie kwenye wadhifa huo hadi ifikapo mwaka, 2026.

Kadri aliteuliwa baada ya fainali za AFCON 2021 na mwenye umri wa miaka 52 aliiongoza Tunisia kufuzu kwa Kombe la Dunia la 2022, ambapo walitolewa hatua ya makundi.

Wenyeji Ivory Coast walimfukuza Kocha, Jean-Louis Gasset, mapema Jumatano, ingawa Tembo hao wamefuzu hatua ya 16 bora kama moja ya timu nne zilizomaliza kwenye nafasi ya tatu bora.



Beki wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Haji Mnoga (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), katika mechi ya Kundi F ya Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), iliyochezwa juzi usiku. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: TFF**

# Madrid yaongoza kwenye mapato

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imetajwa kuwa klabu ya soka iliyoingiza mapato ya juu zaidi duniani kwa msimu wa 2022/23 kwa mujibu wa Deloitte's Sports Business Group, ikichukua nafasi ya Manchester City iliyokuwa kileleni mwa orodha hiyo.

Deloitte Football Money iko katika mwaka wake wa 27 wa kuchanganua klabu za kandanda zinazoingiza mapato ya juu zaidi duniani, na iliripoti Madrid ilipata rekodi ya euro bilioni 10.5 katika msimu wa 2022-23, sawa na ongezeko la asilimia 14 kutoka mwaka jana.

Madrid kwa mara ya mwisho walikuwa kileleni mwa orodha hiyo miaka mitano iliyopita, na waliripoti rekodi ya euro milioni 831 kwa kipindi cha msimu uliopita, zaidi ya mwaka uliopita.

City walipata pungufu ya euro milioni tano kuliko Madrid katika nafasi ya pili, huku tano bora wakijazwa na Paris Saint-Germain (euro milioni 802), Barcelona (euro milioni 800), na Manchester United (euro milioni 746).

Kupanda kwa PSG na Barca katika tano bora kunaonyesha klabu za Ulaya "kurejea" kwenye himaya dhidi ya zile za Ligi Kuu England, kwa mujibu wa Deloitte, ingawa Liverpool, Arsenal, Chelsea na Tottenham Hotspur zote zipo kwenye 10 bora.

Liverpool ndio walioshuka daraja katika orodha hiyo, wakitoka nafasi ya tatu hadi ya saba, kutokana na kushuka kwa matokeo katika michuano ya ndani na Ulaya.

Newcastle United na West Ham United zipo katika nafasi ya 17 na 18, mbele ya mabingwa watetezi wa Serie A, Napoli.

Deloitte alisema takwimu hizo zilifichua kuwa mapato ya kibiashara yamechukua nafasi ya fedha za matangazo kama njia kubwa zaidi ya mapato kwa klabu kwenye orodha kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2015-16, ukiondoa msimu wa 2019-20 ulioathiriwa na COVID-19.

"Mwaka mwingine wa kuvunja rekodi kwa klabu unawakilisha uwezo wa kifedha unaoendelea wa tasnia ya kandanda," alisema Tim Bridge, mshirika mkuu katika Kundi la Biashara la Michezo la Deloitte.

"Mahitaji makubwa ya michezo ya moja kwa moja yanaelekeza kwenye ukuaji zaidi wa mapato ya kibiashara na siku ya mechi. Kwa vile klabu zinaonekana kutoweza tena kutegemea ukuaji wa mapato ya matangazo, kuunda mtindo wa kibiashara unaozingatia zaidi biashara kutazisaidia kufikia mafanikio makubwa na kudhibiti utulivu wao wa kifedha."

Huu ni mwaka wa pili Deloitte kuchambua mchezo wa wanawake -- ingawa takwimu hazijumuishi masoko makubwa kama vile Marekani na Japan kwani data ya klabu hizo haikutolewa.

HABARI MICHEZO

# Stars yaweka rekodi Afrika, yapongezwa

INATOKA UK. 24

kwa kidogo walichokipata.

"Mashindano yalikuwa mazuri, kundi letu lilikuwa gumu, tunashukuru kwa hata hiki kidogo tulichokipata," alisema Fei Toto.

Dismas Novatus, kiungo mkabaji, alisema wachezaji wa timu hiyo hawajafurahi kutolewa katika michuano hiyo, lakini wanachofurahi ni kuweka rekodi ya kupata pointi mbili hatua ambayo hakijawahi kufikiwa huko nyuma.

Novatus alisema wanaondoka katika mashindano hayo wakiwa wamejifunza mambo mbalimbali na sasa wanakwenda kujipanga kwa ajili ya fainali za mwaka 2025.

"Sijui kama tulishawahi kupata hata pointi mbili kwenye AFCON yoyote hatua ya makundi, nadhani ni mwanzo mzuri kuelekea fainali nyingine, " Novatus alisema kwa kifupi.

Wakati huo huo makocha na wachezaji wa zamani wa timu hiyo wamesema ushiriki wa Stars ni sehemu ya kujifunza kuelekea maandalizi ya kuandaa fainali za mwaka 2027 ambazo zinaandaliwa na nchi tatu za Tanzania, Kenya na Uganda.

Nyota wa zamani wa Stars, Adolf Richard, alisema anaungana na Kocha Mkuu wa timu hiyo aliyesimamishwa, Adel Amrouche, kuwa fainali za mwaka huu zililenga zaidi kujifunza na kujenga timu.

"Haya mashindano ni magumu sana, tuwapongeze wachezaji wetu kwa kupambana katika mechi mbili na kuvuna alama mbili, kwa timu yetu ilivyo nilikuwa naamini tunaenda kujifunza na kuandaa kikosi kuelekea msimu wa mwaka 2027 ambao tunakuwa wenyeji," alisema Adolf.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema kulingana na alivyokiona kikosi cha Stars na timu walioicheza nazo, anawapongeza wachezaji kwa matokeo waliyopata.

Katwila alisema kwa sasa Tanzania ilienda kushiriki na kujifunza, michuano hii imewasaidia makocha kuongeza kitu na kurudi nchini kwa ajili ya kutathimini na kufanyia kazi.

"Wachezaji wapongezwe wamepambana sana, wachezaji wazawa kwenda kucheza soka la kulipwa ina faida kubwa sana, lakini tunahitaji kuangalia wachezaji hao kwenda katika timu zitakazowaongezea ushindani ili kuja kusaidiana na wale wanaocheza ligi ya ndani," alisema Katwila.

Amri Kiemba, alisema kulingana na soka letu, Tanzania imepiga hatua kubwa katika miaka hii mitano, haikuwa na matarajio ya kufika mbali katika fainali hizi na mategemeo yake ni kuona wachezaji wanaenda kujifunza.

"Safari hii tumeenda kupata somo, kupoteza mechi moja na kutoka sare mbili si jambo ndogo sana. Tuache lawama kwa wachezaji, tuanzie hapa tulipoishia kwa kuandaa timu kwa ajili ya fainali za 2027," alisema Kiemba.

# NBC YAJITOSA MASHINDANO YA WAITARA TROPHY 2024

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa Sh. milioni 30 kwa ajili ya kudhamini mashindano ya gofu maarufu 'NBC Waitara Trophy 2024' yenye lengo la kukuza na kuendeleza mchezo huo sambamba na kumwenzi mwasisi wa michuano hiyo, Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali, George Waitara.

Mashindano hayo ya siku moja yatafanyika kesho kwenye viwanja vya Gofu vya Lugalo jijini, Dar es Salaam na wachezaji zaidi ya 170 kutoka ndani na nje ya nchi watashiriki. Akizungumza jijini jana, Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa NBC, David Raymond, alisema udhamini wa benki hiyo katika mashindano hayo ni mwendelezo wa jitihada zake za kukuza sekta ya michezo nchini ili kuibua vipaji, kuchochea ajira na kuitumia vyema sekta hiyo katika kutangaza utalii wa ndani.

**"Kwetu ni heshima kubwa kuwa sehemu ya mashindano haya muhimu. Tunaamini udhamini huu utasaidia kuendeleza mchezo wa gofu na pia kuenzi mchango wa Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali George Waitara katika kukuza na kuendeleza mchezo huu," alisema Raymond.**

Aliongeza ushiriki wa wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi utasaidia kuchochea sekta ya utalii, muunganiko wa kibiashara miongoni mwa washiriki pamoja na kutoa fursa kwa wageni kujifunza zaidi mbinu za mchezo huo.

"Zaidi tunaahidi kuendelea kushirikiana na klabu ya gogu ya Lugalo na wadau wengine wa mchezo huu kuhakikisha mashindano yanaendeshwa kwa mafanikio makubwa kama ambayo tunaendelea kushuhudia maendeleo kwenye michezo mingine tunayoidhamini na kuiandaa ikiwamo Ligi Kuu ya NBC Tanzania, NBC Championship na mashindano ya riadha ya kila mwaka ya NBC Dodoma Marathon," alisema mwakilishi huyo.

Naye Meneja wa Klabu ya Gofu Lugalo, Kanali David Mziray, alisema zaidi ya wachezaji 170 watashiriki mashindano hayo mwaka huu wakiwamo vijana wadogo wa shule (Junior).

"Mpaka sasa mwitikio wa wanaotaka kushiriki ni mkubwa, zaidi ya watu 118 kutoka ndani na nje ya nchi wameshathibitisha na maandalizi yanakwenda vizuri ikiwamo ubora wa viwanja ambavyo vitatumika kwenye shindano hilo," alisema Mziray.

Alitoa wito kwa wadau zaidi wa mchezo huo kuendelea kuthibitisha ushiriki wao katika mashindano hayo ya mwaka huu.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko NBC, David Raymond (katikati) akizungumza kuhusu udhamini wa mashindano gofu ya 'NBC Waitara Trophy 2024' yatakayofanyika kesho kwenye viwanja vya Klabu ya Gofu vya Lugalo, Dar es Salaam. Kushoto ni Meneja wa klabu mwenyeji, Kanali David Mziray. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga Princess, Bunda Queens kazini Ligi Kuu*

Na Saada Akida

TIMU ya Yanga Princess inatarajia kuivaa Bunda Queens kutoka mkoani Mara katika mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake itakayochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Yanga Princess inashuka dimbani baada ya kupoteza mechi tatu mfululizo, ikichapwa dhidi ya Simba Queens, Ceasiaa Queens na JKT Queens.

Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, alisema baada ya kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake ikiwamo makosa ya mchezaji mmoja mmoja, anaimani leo hawatarudia katika mechi ya leo.

Haalubomo alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu wapinzani wao pia wamejiandaa vizuri huku wakishuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kupata sare.

"Tumejiandaa vizuri ikiwamo safu ya ulinzi na ushambuliaji kutumia nafasi zinazopatikana ili kupata bao, tunawaheshimu sana Bunda Queens na wachezaji wangu wapo tayari kwa mchezo huo," alisema kocha huyo.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Simba Queens kuwakaribisha Alliance Girls kutoka Mwanza wakati Ceasiaa Queens ambao ni wababe wa Yanga Princess watawaalika Baobab Queens,

Fountain Gate Princess itacheza dhidi ya vinara na mabingwa watetezi, JKT Queens wakati Amani Queens itawavaa Geita Gold Queens.

# Msuva arejea Saudi Arabia

INATOKA UK. 24

andaa kwenda kuitumikia timu yake mpya katika ligi ya Saudi Arabia ambayo anaifahamu baada kumaliza majukumu ya Stars.

"Nafurahi kupata timu na kurejea katika Ligi ya Saudi Arabia, huko ndio nitakapoonekana kwa sasa, kuna ofa nyingi zilikuja kutoka ndani na nje ya Tanzania, Al Najma walikuwa na ofa nzuri," alisisitza Msuva.

Al Najma ni timu ya tano kwa nyota huyo tangu alivyoondoka Yanga katika msimu wa 2017/18 akianza kuichezea Difaa El Jadida na Wydad Casablanca zote za Morocco, Al Qadsiah (Saudi Arabia) na JS Kabylie ya Algeria.

Michezo
Ijumaa Januari 26, 2024
Nipashe



Algeria, Tunisia zatimua makocha UKURASA 22



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva (kushoto), akimtoka beki wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), katika mechi ya Kundi F ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), iliyochezwa juzi usiku nchini Ivory Coast. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: TFF**

# Stars yaweka rekodi Afrika, yapongezwa

## Wafunguka haikuwa na bahati, yapata darasa...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

REKODI imeandikwa. Licha ya kushindwa kusonga mbele, Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), imeweka rekodi ya kuvuna pointi mbili katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) huku wachezaji wa timu hiyo wakisema hawakuwa na bahati.

**Kwa mara ya kwanza Taifa Stars ambayo imeshiriki kwa mara ya tatu fainali za AFCON, mwaka huu imemaliza mechi za hatua ya makundi ikipata sare mbili, sawa na Zambia iliyoshika nafasi ya tatu katika Kundi F.**

Stars ilianza fainali hizo kwa kupokea kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Morocco lakini ikalazimishwa sare ya jioni ya bao 1-1 dhidi ya Zambia na juzi usiku ilimaliza dakika 90 ikiwa suluhu na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Mara ya kwanza Stars ilicheza fainali hizo mwaka 1980 nchini Nigeria, ilimaliza Kundi A ikipoteza michezo miwili na kupata sare moja, ambayo ilikuwa ni dhidi ya Ivory Coast (1-1) wakati fainali za mwaka 2019 zilizofanyika Misri, ikiwa Kundi C ilifungwa michezo yote mitatu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco' alisema timu yake iliwadhibiti vizuri DRC kwa kuziba mianya yao lakini bahati haikuwa yao katika kutumia nafasi walizopata na kufanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bila kufungana.

"Kama nilivyosema awali tunakuja kupambana katika mechi hii na kweli ilikuwa hivyo, niwashukuru sana wachezaji wangu kwa jinsi walivyopambana kadri walivyoweza, bahati haikuwa yetu.

Mchezo ulikuwa mzuri sana, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo wana timu ngumu na wachezaji wenye uwezo, lakini tuliweza kuzuia presha yao, mianya yao yote, tukatengeneza nafasi, ingawa hatukuzitumia na huu ndiyo mpira wenyewe," alisema Morocco.

Naye winga tegemeo wa Stars, Simon Msuva, aliliambia gazeti hili anaona mwanga na mabadiliko makubwa katika kikosi cha timu hiyo na ana imani huko mbele kikosi chao kitaimarika zaidi.

"Tunashukuru kwa sapoti kubwa ya Watanzania wote waliyotuonyesha tangu mwanzo, tumeshindwa kuingia hatua ya 16 bora lakini kadri siku zinavyozidi kwenda kuna mabadiliko yanaonekana, nadhani huu ni mwanzo mzuri kuelekea katika mashindano mengine yanayofuata, haya yameshapita," Msuva alisema.

Kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' alisema pamoja na kutolewa lakini mashindano yalikuwa mazuri na wanashukuru hata

INAENDELEA UK. 23

# Msuva arejea Saudia

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva, amekamilisha mazungumzo ya kujiunga na klabu ya Al Najma inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza nchini Saudi Arabia, imefahamika.

Uamuzi huo wa Msuva unamaliza tetesi za kurejea nchini kujiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ambao walitajwa kuhitaji huduma ya nyota huyo.

Hata hivyo Yanga inadaiwa iliamua kuachana na Msuva katika usajili wa dirisha dogo kutokana na dau alilowaambia wampatie ili ajiunge kwa mara nyingine na klabu hiyo ya Mitaa ya Twiga na Jangwani.

Msuva aliliambia Nipashe jana ameamua kwenda Saudia Arabia baada ya Waarabu hao kumpatia ofa nzuri kuliko timu nyingine za ndani na nje ya Tanzania.

Nyota huyo alisema pia mazingira ya Saudi Arabia ambako aliwahi kucheza, yamepelekea kukubali ofa ya Al Najma ambayo imeridhishwa pia na kiwango alichokionyesha katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zinazoendelea huko Ivory Coast.

"Ni kweli kulikuwa na klabu mbalimbali zinanihitaji za nje ya nchi na hata Tanzania, lakini timu hiyo (Al Najma), ndiyo iliyoleta mezani dau nono zaidi na mimi kuamua kusaini. Nashukuru AFCON imesaidia kunipa timu, ndio maana nilisema nisubiri kwanza," Msuva alisema.

Aliongeza kwa sasa anaji-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >